

IPANGILIO WA NGELI: ULINGANISHI WA NGELI ZA
KISWAHILI SANIFU NA KIKIKUYU CHA KIAMBU.

Na: DAVIES MUTHONDU MUKURIAH

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi
ya mahitaji ya "Master of Arts" katika Chuo
Kikuu cha Nairobi."


1987



UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

UNGAMO


"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na
haijatolewa kwa mahitaji ya Digrii katika
Chuo kingine chochote."



DAVIES MUTHONDU MUKURIAH

(Kitahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini
yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo
Kikuu."



PROF. KAREGA MUTAHI

DNT. MOHAMED FAYARI

TABARUKU

Nawatabarukia kazi hii mke wangu Millicent
Wanjirũ na binti yangu Wanjikũ, babangu:
dada na ndugu zangu.

YALIYOMO

ukurasa

Ungamo	
Tabaruku	
Yaliyomo.....	i
Shukrani.....	iv
Muhtasari.....	vi

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi wa Utafiti.....	1
1.1 Somo la Utafiti.....	1
1.2 Lugha na Watu.....	1
1.3 Madhumuni ya Somo hili.....	2
1.4 Upeo wa Somo hili.....	3
1.5 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili..	4
1.6 Sababu za kulichagua somo hili..	15
1.7 Msingi wa Nadharia.....	17
1.8 Njia za Utafiti.....	19
Tanbihi.....	22

SURA YA PILI

2.0.0 Mpangilio wa Ngeli za Kiswahili.	24
2.1.0 Ngeli ya Kwanza.....	24
2.2.0 Ngeli ya Pili.....	29
2.3.0 Ngeli ya Patu.....	35
2.4.0 Ngeli ya Nne.....	40
2.5.0 Ngeli ya Tano	45

	<u>ukurasa</u>
2.6.0 Ngeli ya Sita.....	50
2.7.0 Ngeli ya Saba	55
2.8.0 Ngeli ya Nane.....	60
2.9.0 Ngeli ya Tisa.....	64
2.10.0 Ngeli ya Kumi.....	71
2.11.0 Ngeli ya Kumi na moja.....	75
2.14.0 Ngeli ya Kumi na nne.....	79
2.15.0 Ngeli ya Kumi na tano.....	83
2.16.0 Ngeli ya Kumi na sita.....	89
2.17.0 Ngeli ya Kumi na saba.....	92
2.18.0 Ngeli ya Kumi na nane.....	95
Tanbini.....	98

SURA YA TATU

3.0.0 Mpangilio wa ngeli za Kikikuyu.	100
3.1.0 Ngeli ya Kwanza.....	100
3.2.0 Ngeli ya Pili.....	104
3.3.0 Ngeli ya Tatu.....	108
3.4.0 Ngeli ya Wne.....	112
3.5.0 Ngeli ya Tano.....	116
3.6.0 Ngeli ya Sita.....	120
3.7.0 Ngeli ya Saba.....	124
3.8.0 Ngeli ya Nane.....	131
3.9.0 Ngeli ya Tisa.....	135
3.10.0 Ngeli ya Kumi.....	140

	<u>ukurasa</u>
3.11.0 Ngeli ya Kumi na moja.....	144
3.12.0 Ngeli ya Kumi na mbili.....	148
3.13.0 Ngeli ya Kumi na tatu.....	152
3.14.0 Ngeli ya Kumi na nne.....	155
3.15.0 Ngeli ya Kumi na tano.....	159
3.16.0 Ngeli ya Kumi na sita.....	163
3.17.0 Ngeli ya Kumi na saba.....	166
Tanbihi.....	169

SURA YA NNE

4.0.0 Ulinganishi wa Ngeli za Kiswahili na za Kikikuyu.....	170
4.1.0 Utangulizi.....	170
4.1.1 Idadi za ngeli.....	170
4.1.2 Wiano wa Kisarufi.....	171
4.1.3 Misingi ya Kimaana.....	181

SURA YA TANO

5.1.0 Hitimisho.....	188
5.1.1 Mapendekezo.....	193
Tanbihi.....	195
Marejeleo.....	196

SHUKRANI

Kufanikiwa kwangu katika kuimaliza kazi hii kulitokana na jitihada za watu wengi. Kwa hivyo nimewajibika kuwatolea shukrani zangu za dhati baadhi ya watu hao.

Kwanza kabisa nawashehenezea shukrani wahadhiri na wasimamizi wangu Prof. Karega Mutahi ambaye pia ni Mudiri wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika, na Dkt. Mohamed Bakari. Wao walinipa fikira nzuri za kitaaluma na pia wakanipa ilhamu nilipokaribia kukata tamaa. Prof. Karega alijitahidi kuipitia miswada ya kazi yangu haraka na kwa uangalifu japo alikuwa na kazi nyingi za idara.

Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kwa kukubali kuyajibu maswala yangu nilipowaendea. Zipokeeni shukrani zangu Prof. Mohamed Abdulaziz, Prof. Lucia Omondi; Dkt. Jay Kitsao, Dkt. Okoth Okombo, Bw. Kazungu Kadenge, Bw. Kithaka wa Mberia, Bi. Judith Nyaga, na Bi. J.H. Oduol.

Nawashukuru sana wanafunzi wazamili wenzangu: Kimani wa Njogu, Bi. Miriam Mwita, Esther Maringah, Bi. Angeline Kioko, na Tom Onditi. Ushirikiano wenu kwa muda tuliosoma pamoja umeniwezesha kuivuka bahari hii yenye mawimbi makali.

Naishukuru pia Serikali ya Ujerumani Magharibi kupitia shirika la German Academic Exchange Services (DAAD) kwa kuyagharinia mambo yote yaliyohusiana na masomo yangu ya uzamili. Wafanyakazi wa shirika hilo walioko Centro House, Westlands walinihudumia haraka nilipouhitaji usaidizi wao.

Nawashehenezea shukrani mke wangu mpendwa Millicent Wanjirũ na binti yangu Wanjikũ. Mliuvumilia upweke mwingi nilipokuwa nimezama masomoni. Ahsanteni sana kwa mapenzi yenu.

Nawashukuruni sana babangu mzee Mukuria Gakami, ndugu na dada zangu, kwa jinsi mlivyoniunga mkono na kunimotisha nilipokuwa nikiishughulikia kazi ya usomi. Ningependa hasa kukutolea shukrani maalum kaka Charles Kamĩri kwa usaidizi wa hali na mali ulionipa tangu nilipokuwa katika kidato cha kwanza. Tasnifu hii ni kilele cha jitihada zako.

Zipokee shukrani zangu Bi. Jane W. Mutharia kwa kukubali kuipiga taipu tasnifu hii na kuitekeleza kazi hiyo vizuri kabisa.

MUHTASARI

Katika tasnifu hii, tumeuangalia uainishaji wa ngeli kama unavyojitokeza katika Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu. Kwa hivyo tasnifu hii imejikita katika sarufi linganishi.

Sura ya kwanza, ni utangulizi wa utafiti. Mambo yaliyojadiliwa katika utangulizi huo ni: Somo la utafiti, Lugha na watu, madhumuni ya somo tunalolishughulikia, upeo wa somo, na yaliyoandikwa kuhusu somo tunalolishughulikia. Pia katika sura hiyo tumezitoa sababu zetu za kulichagua some letu, msingi wa nadharia tulioitumia, na vilevile njia za kufanyia utafiti.

Sura ya pili imezishughulikia ngeli za Kiswahili sanifu. Katika sura hiyo, tumejadili kuhusu idadi ya ngeli zilizoko katika Kiswahili sanifu. Pia tumeonyesha jinsi majina ya lugha hiyo yanavyohusiana na vipande vingine vya sarufi. Misingi ya kimaana inayodhihirika katika ngeli za Kiswahili sanifu pia imejadiliwa.

Katika sura ya tatu, tumezijadili ngeli za Kikikuyu. Mbinu zilizozingatiwa katika kuzieleza ngeli hizo ni sawa na zile zilizovumiwa katika sura ya pili. Yaani misingi ya kimaana na wiano wa kisarufi.

Katika sura ya nne tumetoa ulinganishi wa ngeli kama unavyojitokeza katika lugha mbili tulizozishughulikia. Tumejadili jinsi ngeli za lugha hizo zinavyofanana na kutofautiana. Ulinganishi wetu umezingatia wiano wa kisarufi na misingi ya kimaana.

Sura ya tano ni hitimisho la utafiti wetu. Katika sura hiyo, tumezijadili kauli muhimu zilizotokea na kujadiliwa katika sura zilizotangulia. Aidha, ni katika sura hiyo ambapo tumeyatoa maperdekezo kuhusu utafiti unaoweza kufanywa juu ya mpangilio wa ngeli za Kibantu.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA UTAFITI

1.1 SOMO LA UTAFITI

Katika tasnifu hii, tumezichunguza na kuzilinganisha mbinu zinazotumiwa katika kuziainisha ngeli za Kiswahili sanifu na lahaja ya Kikikuyu inayozungumzwa na wakazi wa wilaya ya Kiambu.

1.2 LUGHA NA WATU

Msingi wa Kiswahili sanifu ni lahaja ya Unguja (Zanzibar) lakini kwa vile Kiswahili sanifu kinatumiwa na watu wengi wenye tofauti za kitamaduni, kiuchumi, na kisiasa, kimeathiriwa sana na msamiati kutoka lugha mbalimbali. (Zawawi, 1979:36).

Ni vigumu sana kuifahamu idadi kamili ya watu wanaozungumza Kiswahili. Hii ni kwa sababu wazungumzaji wa lugha hiyo wametapakaa, wengi wao wakiwa na lugha za kwanza zilizohitilafiana. Watu kama hao hukitumia Kiswahili kama lugha sambazi.

Idadi ya watu wanaozungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza au ya pili inakisiwa kuwa kati ya milioni arobaine hadi hamsini (Myachina, 1981:1).

Kiswahili chatumiwa kama lugha ya kwanza na wakazi wa mwambao wa Afrika Mashariki kuanzia Somalia upande kaskazini hadi visiwa vya Komoro upande wa kusini.

Kiswahili kimeenea sana sehemu za bara hadi kufikia Afrika ya kati na ndipo chasemekana kuwa mojawapo kati ya lugha za Kiafrika zilizoenea zaidi barani Afrika. (Bakari 1982:5).

Kulingana na hesabu ya watu nchini Kenya ya mwaka 1979, lahaja ya Kikikuyu cha Kiambu ilikuwa ikuzungumzwa na takribani watu 686,290.¹ Tukichukulia kwamba idadi ya watu nchini Kenya huongezeka kwa asilimia nne kila mwaka, twaweza kukisia kwamba lahaja hiyo kwa sasa inazungumzwa na takribani watu 903,110.

Chambilecho Mutahi (1979), Kikikuyu cha Kiambu ni sehemu ya lahaja ya kusini kulingana na uainishaji wake wa lahaja za Kikikuyu. Lahaja hiyo ndiyo inayojitokeza kama Kikikuyu sanifu. Hii ni kwa sababu inazungumzwa na watu wengi zaidi kuliko lahaja nyingine. Aidha lahaja hiyo ndiyo inayotumiwa katika maandishi, kufundishia lugha ya Kikikuyu na katika matangazo ya Kikikuyu ya Sauti ya Kenya.

1.3 MADHUNUNI YA SOMO HILI

Somo hili limeushughulikia uainishaji wa ngeli za Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu. Dhamira yetu maalum ni kuzichunguza njia mbili maalum zilizowahi kutumiwa kwa minajili ya kuonyesha mantiki inayoutawala uainishaji wa ngeli. Njia hizo mbili

ni uzingatifu wa viambisho vya majina, na ya pili yazingatia misingi ya kimaana.

Mbinu inayozingatia viambisho ni ya Kimuundo. Kwa hivyo yashikilia kwamba kiambisho kilichoko kwenye jina hukaririwa kwenye vipande vingine vya sarufi ambavyo hutawaliwa na jina. Dhana hiyo inashikiliwa na wanasarufi kama vile Ruzicka (1956: 88), Mbaabu, (1978:33) Welmers (1973:159), Barlow (1960:14), Zawani, (1979:8) na wengineo.

Kundi la pili la wanasarufi lang'ang'ania kwamba makundi ya ngeli huainishwa kwa kutumia misingi ya kimaana. Kwa mfano Ashton, (1947) anasema;

"Kila mojawapo ya ngeli inahusiana na dhana moja au zaidi. Kwa hivyo, majina yenye m- katika uchache na wa- katika wingi yamhusu binadamu"²(Tafsiri yetu)

Kutokana na tofauti zilizozuka kati ya wanasarufi, tasnifu hii imezichunguza baadhi ya kauli zilizotolewa kwa minajili ya kuufikia uamuzi unaofaa.

1.4 UPEO WA SOMO HILI

Somo hili limejishughulisha tu na mambo yanayohusu mpangilio wa ngeli huku ikijikita kwenye

Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu.

Tumejitahidi kuyazingatia maswala muhimu yanayohusiana na vigezo vinavyotumiwa katika uainishaji wa ngeli za Kiswahili sanifu na Kikikuyu. Tumeangalia ni kwa kiasi gani kila mojawapo ya vigezo vilivyotumiwa kinavyoelekea kuyasuluhisha maswala kuhusu uainishaji wa ngeli.

Somo hili pia limejishughulisha na vipande vya sarufi kama vile sifa, idadi, vitenzi, na kadhalika na kuchunguza jinsi vipande hivyo vinavyoathiriwa na jina katika sentensi.

Uchunguzi wa vipande vya sarufi vilivyotajwa una mantiki kwa sababu kama ilivyodokezwa hapo awali, jina hujithahirisha kwenye vipande vingine vya sarufi.

Welmers (1973:173) amewasilisha kauli kwamba lugha za Kibantu kama vile Kiswahili na Kikikuyu zina takiriri za viambisho kwenye vipande vya sarufi. Tumeihakiki kauli hiyo katika sura ya tano (sehemu 5.1.0),

1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kazi nyingi zimewahi kuandikwa kuhusu uainishaji wa ngeli za Kibantu kwa jumla baadhi yazo zikiwa zashughulikia Kiswahili na Kikikuyu. Kazi hizo zimetokea kama vitabu vilivyochapishwa, majarida, na

hata tasnifu katika viwango mbalimbali.

Karibu kazi zote zilizoandikwa kuhusu Kiswahili na Kikikuyu huwa hazina budi kugusia ngeli. Hii ni kwa sababu jina ni kipande muhimu sana katika sarufi za lugha za Kibantu. Kwa hivyo, kazi zilizotajwa katika tasnifu hii ni baadhi tu ya zile zilizochukuliwa kuwa muhimu sana.

Krapf (1850 na 1882) alivitambua vikundi vinane vya ngeli za Kiswahili. Alivihusisha vikundi hivyo na viambisho ili kuonyesha uchache na wingi wa majina yaliyo katika vikundi hivyo.

Kazi ya kwanza ya Krapf iliyashughulikia maswala mengi kuhusu sarufi ya Kiswahili zikiwemo ngeli. Nayo kazi ya pili ilikuwa kama kamusi lakini kwa muhtasari iligusia ngeli.

Krapf aliiona dhana ya maana kwenye ngeli ya kwanza pekee ambayo alisema kuwa ina majina ya viumbe.

Steere (1870) aliziainisha ngeli za Kiswahili katika makundi tisa. Alionyesha viambisho katika baadhi ya makundi hayo na alipokosa viambisho, alitumia majina kama mifano. Steere alimwiga Krapf kwa kuyaorodhesha pamoja majina ya uchache na wingi wa kundi moja. Hata hivyo, Steere hatoi dhana ya maana katika uainishaji wake.

Bleek (1869) alitumia nambari katika uainishaji wake huku akiziandamanisha na viambisho kama vilivyotumiwa na Krapf pamoja na Steere. Tofauti kubwa iliyopo haina ya Steere na akina Krapf ni kwamba yeye (Bleek) aliuchukulia uchache na wingi kuwa katika makundi tofauti. Bleek alivitambua vikundi kumi na vitano vya ngeli katika Kiswahili.

Wanasarufi wa baadaye waligawanyika. Baadhi yao waliitumia misingi iliyowekwa na Krapf pamoja na Steere. Wengine walitumia mbinu iliyozushwa na Bleek.

Baadhi ya wanasarufi walioizingatia mbinu ya Krapf na Steere ni kama vile Burt, (1917); Broomfield (1931); Ashton, (1944); Loogman, (1965), Brain, (1966) Der- Houssikian; (1969); Wilson; (1970), na Welmers (1973).

Wanasarufi walioitumia mbinu ya nambari ingawa waliandamanisha na viambisho ni kama vile Polome; (1967); Mbaabu (1978); Myachina; (1981) na wengineo.

Burt (1917) aliyatambua makundi kumi ya ngeli za Kiswahili na akajaribu kuvihusisha viambisho na ~~maana~~. Aliyaweka majina yanayohusiana na binadamu kwenye ngeli ya kwanza (m-, wa-) na akayaweka ya wanyama kwenye ngeli ya tatu (N-, N-).

Burt ameyaorodhesha majina kama vile "yahudi", "hajiri", "shekhe", na "kuhani" kwenye ngeli ya tano iliyo na viambisho (ji- ma-) ingawa amesema kwamba ngeli ya kwanza ndiyo inayomhusu binadamu (1917:122).

Broomfield (1931) aliziorodhesha ngeli za Kiswahili katika makundi manane. Lakini mwanasarufi huyo hagusii kuhusu misingi ya kimaana katika kikundi chochote kile. Hata hivyo, Broomfield amejitahidi kuyaelezea mabadiliko ya sauti ambayo yanatokea kwenye viambisho vya majina.

Kazi ya Ashton, (1944) ni mojawapo ya zile zilizopiga hatua katika kuelezea misingi ya kimaana inayoambatana na viambisho vya ngeli za Kiswahili.

Loogman (1965) aliziorodhesha ngeli za Kiswahili katika makundi manane. Ametumia jozi za viambisho ili kuonyesha uchache na wingi. Aidha, Loogman ameyahusisha baadhi ya makundi ya ngeli na maana. Ameviweka vikundi vya mahali (pa, mu, ku) katika kundi moja.

Brain (1966) aliyatambua makundi sita ya ngeli za Kiswahili na akajitahidi kukipa kila kikundi misingi ya kimaana. Hata hivyo, Brain aonekana kuwa amekanganyika asemapo kwamba ngeli ya m- wa- ina majina ya binadamu na kisha kutoa mifano kama vile

"kiboko" na "kifaru" katika ngeli ya ki-, vi- (1966:19) Brain pia ameyaweka majina ya wanyama kama vile "ndege", "ng'ombe", "nzige", na "nyoka" katika kikundi akiitacho N-.

Kazi ya Wilson (1970) haitofautiani sana na ya Brain isipokuwa kwamba Wilson ameyatambua makundi saba ya ngeli za Kiswahili.

Katika tasnifu yake ya Ph.D, Der- Houssikian (1969) aliushughulikia uainishaji wa ngeli za Kimvita (Kimombasa). Katika kazi hiyo, Der-Houssikian alivitambua vikundi saba vya ngeli. Aliiona misingi ya kimaana katika kikundi cha kwanza pekee ambacho anakiita mu-, wa-. Inathahirika kwamba mwanasarufi huyo ameathiriwa sana na kazi za Ashton na Polome.

Kazi ya Der - Houssikian ni ya kipekee ikilinganishwa na nyingine. Hii ni kwa sababu inalizingatia swala la ngeli pekee ilhali kazi nyingine zilizotajwa hapo awali zinazingatia sarufi kwa jumla na kutajia kijuujuu tu mambo yanayohusiana na ngeli.

Polome (1967) ametumia nambari pamoja na viambisho katika kuziainisha ngeli za Kiswahili. Ngeli ni mojawapo tu kati ya maswala ya kisarufi aliyoyashughulikia katika kitabu chake kiitwacho Swahili Language Handbook.

Polome ameathiriwa sana na mpangilio unaozingatia viambisho vya majina. Kauli hiyo yathihirishwa na matumizi yake ya jozi za nambari kwa ngeli zilizo na viambisho sawa. Kwa mfano 11/14 kwa vile zaanzia na {u} , na 15/17 kwa kuwa zina kiambisho {ku} . Aidha Polome ameitoa mifano ya walemavu kama vile "kipofu", "kilema" na "kiziwi" katika ngeli ya saba kwa kuwa majina hayo yaanza kwa mofemu {ki} (1967:98).

Kazi ya Myachina, (1981) inaufuata mkondo wa Polome isipokuwa kwamba imefafanua zaidi kuhusu misingi ya kimaana inayoambatana na uainishaji wa ngeli katika Kiswahili.

Mbaabu (1978) ameathiriwa sana na mbinu iliyotumiwa na Polome hivi kwamba sehemu inayojadili kuhusu ngeli katika kitabu chake kiitwacho Kiswahili Lugha ya Taifa yajitokeza kama tafsiri ya mawazo yaliyowasilishwa na Polome. Hata hivyo, Mbaabu (1985) aliurejelea upya uainishaji wa ngeli aliouzingatia hapo awali baada ya kuuhisi udhaifu wake. Anasema:

"Kwanza kabisa tumeona kwamba mpangilio wa majina katika ngeli hufuata viambisho vya umoja na wingi wa majina. Maelezo hayo hayatoshi kwa sababu majina ambayo yangukuwa

katika jamii au kundi moja
hugawanywa katika ngeli tofauti
kutegemea viambisho vya majina
yenyewe."³

Mbinu aliyoamua kuitumia Mbaabu katika Sarufi ya Kiswahili ili kuujenga upya mpangilio wa ngeli za Kiswahili ni utumiaji wa "viishirio vya karibu na anayezungumza" (1985:98) Mbaabu hatutolei sababu maalum zinazomfanya akitumie kigezo hicho.

Zawawi (1979) alijadili kuhusu maneno yaliyokopwa hasa kutoka Kiarabu yaliyoko katika lugha ya Kiswahili na kuonyesha jinsi yanavyoiathiri sarufi ya Kiswahili. Zawawi ameitoa kauli kwamba maneno yakikopwa kutoka lugha moja hadi nyingine, huuchukua muundo wa lugha inayokopa (1979:143). Zawawi pia ameyachambua na kuyahakiki mawazo yaliyotolewa na baadhi ya wanasarufi waliomtangulia. Kwa mfano Krapf, Steere; Bleek, Meinhof, Marconnes, Ashton; Guthrie, Loogman, na Polome. Ametumia mifano ya kutoka kazi za fasihi na magazeti ili kudhihirisha kwamba majina katika sentensi hayazingatii muundo maalum wa ngeli na kwa hivyo majina hayafai kuwekwa katika makundi maalum!! Kazi za kifasihi alizozitumia Zawawi ni riwaya ya Mohamed Said Abdalla iitwayo

Kisima cha Gini; ya Baalawy ijulikanayo kama Hadithi za Bibi Maahira, na pia tamthilia ya Ebrahim Hussein iitwayo Kinjeketile. Gazeti alilolitumia laitwa Uhuru.

Matumizi ya kazi za kifasihi kama thihirisho la ukweli katika kuelezea sarufi ya lugha ni jambo lililopingwa na Matthews (1974). Matthews asema kwamba si jukumu la mwanasarufi kuyashughulikia mambo ya kimtindo kama vile ukiushi ambayo kwa kawaida hutokea katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mifano aliyoitoe Zawawi haina misingi thabiti ya kisarufi. Hata hivyo maswala aliyoyazusha kuhusu uainishaji wa ngeli yametufaidi sana katika utafiti wetu.

Gibbe (1983) aliandika makala kuhusu ngeli ya kwanza katika Kiswahili. Ingawa makala hayo yameishungulikia sehemu ndogo tu, Gibbe amezitoe kauli muhimu ambazo zingetumiwa katika kuelezea uainishaji wa ngeli za Kiswahili kwa jumla. Gibbe ametoa mifano kadhaa kuonyesha nafasi ya udhananishaji katika uainishaji wa ngeli na kutumulikia udhaifu unaoambatana na uzingatifu wa viambisho vya majina. Anasema:

"Kigezo cha viambishi hakiwezi

kujitosheleza chenyewe, kwani
kuna nomino zisizo na viambisni."

Katika tasnifu yake ya B.A, Mutisya (1986) aliushughulikia ulinganishi wa ngeli za Kiswahili na za Kikamba. Ingawa mojawapo ya malengo yake ni kuonyesha kigezo kinachofaa kutumiwa katika kuziainisha ngeli, Mutisya hatutolei matokeo ya utafiti wake. (1986:9). Hata hivyo kazi yake ina ukwasi wa data iliyotolewa katika majedwali.

Kazi ya Mutisya imetufaidi sana kwa jinsi inavyoelekeana na somo letu. Kazi hiyo ni ya kipekee kwa vile inalinganisha mpangilio wa ngeli za lugha mbili na mojawapo ya lugha hizo, Kiswahili ni moja kati ya zile tunazozishughulikia. Nayo lugha ya Kikamba haitofautiani sana na Kikikuyu chambilecho Bennet (1967:127).

Ni kazi chache tu za kitaaluma zilizowahi kuandikwa kuhusiana na sarufi ya Kikikuyu. Kazi za mwanzo zilinuiwa kuwasaidia Wazungu waliokuwa wakifanya kazi Ukikuyuni wakati wa enzi za Kikoloni. Mifano ya kazi hizo ni: Gecaga na Kirkaldy (1953); na Leakey (1959).

Kazi hizo mbili zimezungumzia kuhusu sarufi ya Kikikuyu kijuujuu tu. Hata hivyo kazi ya Leakey ina mawazo ya kipekee kuhusu misingi ya kimaana

inayoambatana na uainishaji wa ngeli za Kikikuyu. Misingi hiyo, kama anavyoonyesha Leakey inajikita katika isimu - jamii. Kwa mfano. Leakey anasema kwamba majina yaliyoainishwa katika ngeli ya kwanza huwa yatokana na mizimu. Hatungeweza kusithibitisha kauli za Leakey katika utafiti wetu.

Njoroge (1978) aliushughulikia uundaji wa majina kutokana na vipande vingine vya sarufi hasa vitenzi na sifa. Alitumia jozi za nambari katika kuonyesha jinsi makundi ya ngeli yanavyojitokeza katika Kikikuyu. Utafiti wa Njoroge ulijikita katika lahaja ya Kimathira sawa na ya Ford (1974) ambaye alijadili kuhusu umuhimu wa kiimbo katika lugha ya Kikikuyu.

Chambilecho Leakey (1959:6) kiimbo huwa na umuhimu mkubwa katika lugha ya Kikikuyu kwa kuwa chaonyesha tofauti za maana. Lakini hatukukishughulikia katika tasnifu yetu kwa sababu hakielekei kuuathiri uainishaji wa ngeli.

Mutahi (1977) aliushughulikia uainishaji wa lahaja za **Kibantu** zilizoko kusini mwa mlima Kenya. Amegusia kuhusu ngeli asemapo kwamba uainishaji wa ngeli kwa kiasi huzingatia wiano wa kisarufi. Mutahi pia aliongeza kwamba majina yasio na viambisho aghalabu huainishwa kwenye ngeli ya 9/10 isipokuwa

yawe yahusiana na binadamu. Mutahi amesema kuwa kuna jumla ya ngeli kumi na nane katika Kikikuyu (1977:60-61).

Katika tasnifu yake ya M.A., Gathenji (1981) aliandika kuhusu viambisho vifuatilizi katika vitenzi pamoja na mnyambuliko wake katika Kikikuyu. Kazi hiyo imetufaidi kwa sababu inashughulikia mojawapo kati ya vipande vya sarufi ambavyo vinaathiriwa na jina.

Kazi nyingine iliyotufaidi katika utafiti wetu ni ya Wa Mberia (1979). Kazi hiyo imejadili muundo wa jina katika Kitharaka ambayo ni mojawapo ya lugha zilizo katika eneo moja na Kikikuyu. Katika kazi hiyo, Wa Mberia ametuthiirishia kwamba uainishaji wa ngeli za Kitharaka una misingi ya kimaana.

Makala ya Bennet (1970) yalizitahakiki mbinu zilizowahi kutumiwa na wanasarufi wa awali za kuzingatia sana viambisho vya majina pekee. Bennet ametumia herufi "A" hadi "N" na kuziandamanisha na viambisho. Mchango wake mkubwa ni msisitizo wa umuhimu wa kuzingatia wiano wa kisarufi katika kuyajadili mambo yanayohusu uainishaji wa ngeli.

1.6 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO HILI

Sababu zinazotolewa na wasomi wengi kuhusu kinachowabidi kulishughulikia somo fulani la kitaaluma aghalabu huwa zahusiana na kuweco kwa uhaba wa kazi za aina hiyo.

Sababu zetu za kulichagua somo letu hazitokani sana na kuweco kwa uhaba wa kazi zinazozingatia uainishaji wa ngeli. Kazi za aina hiyo hasa kuhusiana na lugha ya Kiswahili zimekuweco kwa muda zaidi ya karne moja kuanzia wakati wa akina Krapf miaka ya 1850 hadi za akina Mbaabu (1985). Lakini kumekuwa na mikabala mingi iliyohitilafiana kama walivyo watu waliushughulikia uainishaji wa ngeli.

Tuliamua kulichagua somo letu kwa minajili ya kuiafikisha mikabala iliyowahi kutumiwa katika uainishaji wa ngeli za Kiswahili na za Kikikuyu. Kutokuweco kwa maafikiano kuhusu mbinu ipasayo kutumiwa kuelezea kipengele muhimu cha sarufi za lugha za Kibantu kwaelekea kuonyesha kwamba lugha hizo hazina mwelekeo.

Inatupasa kuungama kwamba tasnifu yetu haikusudiwi kuyasuluhisha kabisa matatizo yaliyowakumba wanasarufi waliotutangulia. Nia yetu ni kuichangia mijadala iliyowahi kuzuka kuhusu uainishaji wa ngeli katika Kiswahili na Kikikuyu. Chambilecho

Clement Maganga, ni jambo lisilowezekana kwa mtu yeyote yule kudai kwamba ameyatoa maelezo ya kutosha juu ya lugha yoyote ile. Anawambia;

"Hakuna mtu anayeweza kudai kwamba sarufi ya lugha yoyote ile huwa imeelezwa kikamilifu, maana mitazamo hubadilika kutegemea na nadharia inayotumiwa"⁵

Sababu yetu nyingine ya kulichagua somo hili ni kwamba mbinu inayozingatia viambisho vilivyoko kwenye majina pekee katika kuziainisha ngeli imejikita sana katika vitabu vinavyotumiwa kusomeshea ingawa kwa maoni yetu inapotosha. Tumeamua kuumulika udhaifu huo huku tukiwa na matarajio kwamba sarufi haitaendelea kuelezwa jinsi isivyoth^dhirika.

Chambilecho Zawani (1979:99) na Bakari (1982:5) kiini cha udhaifu tulioumulika ni kwamba wanasarufi wa baadaye waliuchukua mkondo wa kuainisha ngeli kama ulivyowekwa na wanasarufi wa kigeni. Wanasarufi hao waliziangalia lugha za Kibantu kwa kuvitumia vigezo vya lugha zao wenyewe ambazo zina miundo tofauti kabisa. Wanasarufi hao wa kigeni aghalabu walizitoa kauli za kijumla sana juu ya mambo yaliyotofautiana.

Gibbe ameonyesha umuhimu wa kuweko kwa utafiti zaidi juu ya uainishaji wa ngeli. Amesema;

"Hatuwezi kusema kuwa mjadala
tuliouendesha ni wa mwisho kuhusu
ngeli, ila tunaweza kusema kuwa
tumejaribu kumulika maswala kadhaa
ambayo hayakushughulikiwa kabisa
au yaliyoshughulikiwa kijuujuu mno,
ili kukaribisha uchunguzi zaidi
katika swala hili muhimu katika
kuelewa vizuri lugha hii (ya Kiswahili)"⁶

Ni matumaini yetu kwamba utafiti wetu utakuwa
mwitikio mwema kwa Gibbe katika kuchangia fikira
zenye mwelekeo juu ya swala kuhusu mpangilio wa ngeli.

1.7 MSINGI WA NADHARIA

Nadharia ni utaratibu unaotumiwa kama dira ili
kuzipa mwelekeo fikira za kitaaluma. Wanasarufi
wamezingatia taratibu mbalimbali kupangia ngeli za
lugha mbili tunazozishughulikia.

Kuna kundi la wanasarufi waliotumia viambisho
vilivyo kwenye majina pekee. Mifano ya wanasarufi hao
ni: Krapf, Steere, Ashton, Der-Houssikian, Burt,
Brain, Loogman; Wilson, na wengineo. Mpangilio huo
una upungufu kwa sababu kuna uwezekano wa majina kuwa
na viambisho sawa lakini wiano wa kisarufi kwenye
vipande vingine ukawa unahitilafiana kabisa.

Njia nyingine iliyowahi kutumiwa katika kuziainisha ngeli hasa za Kiswahili ni ule unaozingatia viambisho vinavyotokea kwenye vitenzi. Njia hii yapendelewa sana na wanasarufi wa Tanzania kama vile Kapinga (1983), na Mdee (1986).

Mbaabu (1985) ameizua njia mpya ya kuziainisha ngeli za Kiswahili. Njia hiyo inazingatia viashiria vya karibu na anayezungumza. Mbaabu anaipendekeza njia hiyo kwa kuwa majina yote ya kundi moja hutumia viashiria sawa (1985:98).

Kila mojawapo ya njia zilizotajwa hapo juu imekitumia kipande kimoja pekee cha sarufi kama kigezo katika kuzipanga ngeli. Matumizi ya kigezo kimoja kama dira ya kuelezea sarufi ni jambo lisilomfaa mwanasarufi. Kauli hiyo imesisitizwa na Bennet (1986) asemapo kwamba;

"Ni jukumu la sarufi kuyapanga maingiliano ya maneno sio maneno kipekee. Tunatarajia kuthahirishiwa jinsi makundi hayo ya maneno yanavyo- jitokeza katika sentensi lakini sio kutolewa orodha ya vipande vya maneno"⁷

(Tafsiri yetu)

Kufuatana na kauli ya Bennet ambayo twaiunga mkono kwa dhati, tasnifu yetu imezingatia jinsi vipande mbalimbali vya sarufi vinavyojitokeza katika sentensi. Vipande tulivyoviangalia ni majina, ^{Nimiliki} slia, vitenzi, vijina vihusishi, idadi, na vimiliki.^{Shu} Kwa ufupi njia yetu inazingatia wiano wa kisarufi.

1.8 NJIA ZA UTAFITI

Tumeufanya utafiti wetu kufuatia njia mbili muhimu. Kwanza tumezipitia kazi mbalimbali zilizowahi kuandikwa juu ya sarufi za Kiswahili na Kikikuyu. Tumejikita sana kwenye kazi zinazojadili kuhusu mpangilio wa ngeli ili kuzipa nguvu kauli zinazotokana na utafiti wetu. Ni kwa kuzipitia kazi hizo ambapo tumeweza kuziona pengo zilizoachwa na wanasarufi waliotutangulia. Tumejitahidi kuzijaza pengo hizo.

Njia nyingine ya utafiti ambayo tumeitumia ni kuyarekodi mazungumzo baina ya watu wanaozizungumza lugha mbili tunazozishughulikia na kuangalia jinsi sarufi inavyojithiirisha. Umuhimu wa utafiti wa aina hiyo unatajwa na kutiliwa mkazo na Zawawi asemapo;

"Ni muhimu kuifikiria sarufi
sivyo kama ilivyokuwa siku
za nyuma au kama wachambuzi
wanavyoifikiria kuwa lakini

kama ilivyo leo"⁸ (Tafsiri yetu).

Tumeutumia ujuzi wetu wa lugha ya Kikikuyu ambayo ndiyo lugha yetu ya kwanza na kuthibitishia usawa wa data yetu kwa kuwauliza wenzetu. Tumeuona umuhimu wa kutumia data kutoka kwa watu ambao hawajaathiriwa sana na miundo ya lugha nyingine. Tuliweza kulisuluhisha jambo hilo kwa kuwahoji wazee hasa walioko sehemu za mashambani.

Kulingana na utafiti alioufanya Bakari (1982) kuhusu uainishaji wa lahaja za Kiswahili, kuna tofauti chache sana za kifonolojia kati ya lahaja ya Kiunguja iliyo msingi wa Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimvita (1982:20). Kwa hivyo ilitufaa kuufanyia utafiti wetu wa ngeli za Kiswahili katika sehemu za Mombasa.

Kauli ya Bakari imeungwa mkono na utafiti wa Der-Houssikian. Data iliyotokana na utafiti huo haina tofauti na zile zilizowahi kupatikana kwenye kazi zilizoandikwa juu ya Kiswahili sanifu ingawa Der-Houssikian aliishughulikia lahaja ya Kimombasa (Kimvita).

Tumezirekodi data za utafiti wetu kwa kuyatumia maandishi ya kifonetiki ambayo yalipendekezwa na shirika la kimataifa la fonetiki mnamo mwaka wa 1949.

Baada ya kuzirekodi data zetu, tumezichambua na kuonyesha jinsi Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu zinavyofanana na kutofautiana.

TANBIHI

1. Kenya Government (1979) Kenya Population Census,
Juzuu la kwanza, Nairobi,
Government Printers. uk. 33
2. Ashton, E.C. (1944) Swahili Grammar, London,
Longman, uk. 10
3. Mbaabu, I. (1985) Sarufi ya Kiswahili, Nairobi
Kenya Publishing and Book
Marketing Company Ltd. uk. 95
4. Gibbe, A.G. (1983) "Uchambuzi wa Nomino za Ngeli
ya kwanza katika Kiswahili"
makala katika Lugha ya
Kiswahili. Dar-es-Salaam;
Taasisi ya Uchunguzi wa
Kiswahili, uk. 246.
5. Maganga, C. (1983) Katika Dibaji ya Kapinga, M.C.
Sarufi Maumbo ya Kiswahili
Sanifu, Dar-es-Salaam;
Printpak Tanzania Ltd. uk. iv
6. Kama 4 hapo juu, uk. 255

7. Bennet, P.R. (1986) "Grammar in The Lexicon"
makala katika, Journal of
Languages and Linguistics;
Juzuu la 7/1, Dordrecht,
Foris Publications; uk.7
8. Zawawi, S.M. (1979) Loan Words and Their Effect
on The Classification of
Swahili Nominals, Leiden,
E.J. Brill.

SURA YA PILI

2.0.0 MPANGILIO WA NGELI-ZA KISWAHILI

Kutokana na utafiti tulioufanya, tumeyatambua makundi kumi na sita ya ngeli. Tumeifikia idadi hiyo kwa kutumia mbinu ya mpangilio wa ngeli iliyopendekezwa na Bleek (1862). Kulingana na mbinu ya Bleek, uchache na wingi wa majina hupangwa katika makundi tofauti.

Makundi yaliyojitokeza ni 1; 2; 3; 4; 5; 6; 7; 8; 9; 10; 11; 14; 15; 16; 17; na 18. Tutaiangalia kila mojawapo ya ngeli zilizotajwa hapo juu ili tuone jinsi majina yanavyoathiriana na vipande vingine vya sarufi. Vipande vitakavyozingatiwa ni viashiria; sifa; vitenzi, vijina vihusishi; idadi na vimiliki.

2.1.0 NGELI YA KWANZA

Ngeli ya kwanza huwa na majina ya viumbe vyote vyenye uhai. Chambilecho Gibbe (1983).

("Kitu ambacho ni muhimu kufikiriwa katika udhananishaji wa ngeli ya kwanza ni 'kukata roho'. Viumbe vyote vinavyokata roho vimo katika ngeli ya kwanza").¹

Umuhimu wa dhana ya uhai katika uainishaji wa majina ya ngeli hii pia umedhihirishwa na Mdee (1986) asemapo:-

("Jambo muhimu katika upatanisho wa m-/wa- ni kwamba jina lazima liwe la mtu, mnyama, au mdudu). Umbo la jina sio kigezo muhimu katika uteuzi wa viambishi vipatanishi"²

Wiano wa kisarufi katika ngeli ya kwanza huwa sawa kulingana na kipande cha sarufi kinachotumiwa hata ikiwa viambisho vilivyo kwenye majina vimetofautiana. Kauli hiyo itadhihirishwa na mifano tutakayoitoa.

2.1.1. VIASHIRIA/KATIKA NGELI YA 1.

Mofemu {^{yu}ju} hutumiwa kama kiashiria cha karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Kiashiria cha karibu na anayesikiliza katika ngeli hii ni {^{yo}jo} . Mofemu {ju} na {jo} pia hutumiwa kama virejeleo ikiwa kitu kinachohusika chajulikana kwa anayezungumza pamoja na anayesikiliza.

Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi majina ya ngeli ya kwanza yanavyochukuana na viashiria.!

- 1) [mtɔtɔ huju hujo juɛ]
[kijana huju hujo juɛ]
[kaɗi huju hujo juɛ]
[kiwɛtɛ huju hujo juɛ]

[bubu	hu <u>ju</u>	hu <u>ju</u>	<u>ju</u> lɛ]
[mbu	hu <u>ju</u>	hu <u>ju</u>	<u>ju</u> lɛ]
[kabwɛla	hu <u>ju</u>	hu <u>ju</u>	<u>ju</u> lɛ]
[pɔka -	hu <u>ju</u>	hu <u>ju</u>	<u>ju</u> lɛ]
[kondɔɔ - kɔndɔ:	hu <u>ju</u>	hu <u>ju</u>	<u>ju</u> lɛ]
[papa -	hu <u>ju</u>	hu <u>ju</u>	<u>ju</u> lɛ]

2.1.2 (SIFA/ KATIKA NGELI YA 1)

Katika ngeli hii, /mofemu {mu} ndiyo inatumiwa ili kuyadhihirisha majina kwenye sifa. (Sauti [u] katika mofemu {mu} hupotea iwapo inafuatwa na konsonanti.)

SHERIA 'A'

u → ∅ / m. - [+k]

Kulingana na sheria ya kifonetiki iliyotolewa hapo juu, sauti [u] hupotea ikiwa imetanguliwa na [m] na kufuatwa na konsonanti yo yote ile.

- 2) [mtɔtɔ mzuri] / mu+zuri /
 [ɲɔmbɛ mkupɔbwa] / mu+kupɔbwa /
 [kiwɛtɛ mɲɔɲɛ] / mu+ɲɔɲɛ /
 [kaɗi mrɛfu] / mu+rɛfu /
 [daktari mfupi] / mu+fupi /
 [kabwɛla mjanja] / mu+janja /

2.1.3 VITENZI/KATIKA NGELI YA 1

Majina huwakilishwa na /mofemu {a} kwenye vitenzi katika ngeli ya kwanza. Kwa mfano.

3) [mtoto]	[alianguka]
[daktari]	[alitutibu]
[mbu]	[aliniuma]
[kiwete]	[aliombewa]
[kuku]	[atatinjwa]
[kijana]	[amefaulu]

2.1.4 KIJINA KIHUSISHI/KATIKA NGELI YA 1

Katika lugha ya Kiswahili, kijina kihusishi hutokea kati ya mofemu inayoonyesha wakati na shina la jina./

Mofemu {jɛ} ndiyo inayotumika kama kijina kihusishi cha ngeli ya kwanza kwa mfano.

4) [mzee]	[alijanguka]
[ngombe]	[alijetinjwa]
[kaŋi]	[atakajehubiri]
[kijana]	[alijefuzu]
[daktari]	[anajefuzu]
[mbu]	[alijeniuma]

2.1.5 (IDADI) KATIKA NGELI YA 1

Kiwakilishi cha jina kwenye idadi katika ngeli hii huwa /mofemu {mu}. Kwa mfano.

- 5) ([mzεε mmɔja]
[ɲmbε mmɔja]
[kaɖi mmɔja]
[kijana mmɔja]
[daktari mmɔja]
[nzigε mmɔja]

2.1.6 (VIMILIKI) KATIKA NGELI YA 1

Mofemu {u} ndiyo inayoyawakilisha majina kwenye vimiliki katika ngeli ya kwanza. (Lakini [u] hubadilika na kuwa nusu vokali [w] inapofuatiwa na vokali zilizoko mwanzoni mwa mashina ya vimiliki). Kutokea kwa [w] kunasababishwa na sheria ya kifonetiki. Kulingana na sheria hiyo, vokali [u] hubadilika na kuwa nusu vokali [w] ikifuatiwa na vokali yo yote ile isipokuwa [u].

SHERIA "B"

$$u \longrightarrow w / - v^3$$

6) [mzɛɛ	wangu]	/u+angu/
[kijana	wako]	/u+ako/
[gombɛ	wakɛ]	/u+akɛ/
[daktari	wɛtu]	/u+ɛtu/
[kaɖi	wɛnu]	/u+ɛnu/
[kɔndɔɔ	waɔ]	/u+aɔ/

Mifano ya majina ya ngeli ya kwanza tuliyoitoa inaonyesha kutofautiana kwa viambisho vya ngeli. Lakini kuna wiano wa kisarufi kulingana na kipande cha sarufi kinachohusika. Kwa mfano:-

7) [mtɔtɔ ; mzɛɛ]	kiambisho ni	{ mu }
[kijana, kiwɛtɛ]	kiambisho ni	{ ki }
[kaɖi, daktari, kabwɛla, kɔndɔɔ]	kiambisho	

ni { ∅ } yaani kapa.

2.2.0 NGELI YA PILI

(Katika Kiswahili sanifu, ngeli ya pili huwa na wingi wa majina ya ngeli ya kwanza.)

Haiwezekani mtu kutaja kuwoko kwa kiambisho maalum kwenye majina ya ngeli hii. Viambisho vitatofautiana ingawa kutakuwa na mkubaliano wa kisarufi. kwa mfano:-

8)

- (i) Majina yenye kiambisho {mu} katika uchache, huwa na {wa} katika wingi
- (ii) Majina yenye {ki} katika uchache huwa na {vi} katika wingi.
- (iii) Majina yenye {∅} katika uchache huwa na {∅} au {ma-} katika wingi.

Kwa mfano:

[kondoo] (uchache); [kondoo] (wingi) {∅}
[karani] (uchache); [makarani] (wingi) {ma}
[daktari] (uchache); [madaktari] (wingi) {ma}

2.2.1 (VIASHIRIA) KATIKA NGELI YA 2

Kwa jumla, majina huwakilishwa na/mofemu {wa} iwapo ashirio ni la karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Ikiwa ashirio ni la karibu na anayesikiliza, mofemu itakayotumiwa ni {∅}. Kwa mfano.

- 9) [wanafunzi - hawa ha∅ walε]
[gombε - hawa ha∅ walε]
[makarani - hawa ha∅ walε]
[vijana - hawa ha∅ walε]
[bubu - hawa ha∅ walε]
[mbu - hawa ha∅ walε]

2.2.2 (SIFA/KATIKA NGELI YA 2

Katika ngeli hii, {mofemu {wa}} ndiyo inayoyawakilisha majina kwenye sifa. Kwa mfano:

10)

[watoto]	[<u>wazuri</u>])
[ngombε]	[<u>wakubwa</u>]
[bubu]	[<u>wanongε</u>]
[viwetε]	[<u>watSanga</u>]
[madaktari]	[<u>wafupi</u>]
[mbu]	[<u>wabaja</u>]

2.2.3 (VIPENZI/KATIKA NGELI YA 2

Majina huwakilishwa na {mofemu {wa}} kwenye vitenzi. Kwa mfano:

11)

[wazεε]	[<u>walianguka</u>]
[madaktari]	[<u>walimhudumia</u>])
[viwetε]	[<u>wanεombεwa</u>]
[kuku]	[<u>wanatipjwa</u>]
[vijana]	[<u>wamεfaulu</u>]
[mbu]	[<u>wamεniuma</u>]

2.2.4 KIJINA KIHUSISHI KATIKA NGELI YA 2

{Mofemu {o}} ndiyo inayotumiwa kama kijina kihusishi kuyawaakilisha majina ya ngeli hii. Kwa mfano:-

12)


[wazεε	wali <u>o</u> anguka]
[madaktari	wali <u>o</u> mhudumia]
[ka <u>di</u>	wana <u>o</u> hubiri]
[viwεtε	wataka <u>o</u> mbewa] ⁴
[vijana	wali <u>o</u> funzu]
[mbu	wana <u>o</u> niuma]

2.2.5 (IDADI) KATIKA NGELI YA 2

(Kiambisho {wa} ambacho huwakilisha jina kwenye idadi katika ngeli ya pili hutokea tu kwenye baadhi ya nambari. Nambari zilizo na kiambisho katika Kiswahili ni mbili; tatu; nne; tano na nane.) Nambari sita, saba, tisa na kumi hazina viambisho. Yaani mofemu ya kiambisho ni kapa, {∅} .

(Neno [wengi] ambalo hutumiwa kuonyesha wingi kijumla katika ngeli ya pili huwa na umbo ta silabi wa+ingi . Vokali [ε] katika [wengi] yatokana na kuungana kwa [a] katika {wa} na [i] katika {-ingi} . Muungano huo hutokana na sheria ya kifonetiki isemayo kwamba vokali ya chini ikifuatana na vokali ya juu hatimaye huwa kuundwa kwa vokali wastani (ya katikati)

SHERIA "C"



Mifano ya uhusiano kati ya majina na kipande cha idadi katika ngeli ya pili ni kama ifuatayo:

13)

- ([wazεε wawili])
- [vijana watatu]
- ([madaktari wannε])
- [wanafunzi watanɔ]
- [kondɔɔ sita]
- [watɔtɔ saba]
- [kaɖi wananε]
- [watʂεzaji wεngi] / wa+ingi /

2.2.6 VIMILIKI KATIKA NGELI YA 2

Kiwakilishi cha jina kwenye vimiliki katika ngeli ya pili ni sawa kabisa na cha ngeli ya kwanza. Yaani ni mofemu {u} .

Kutokana na kufanana kwa vimiliki kati ya ngeli hizo haiwezekani mtu akajua kama jina liko katika hali ya uchache au wingi ikiwa jina linalohusika ni baadhi ya yale yasiyo na viambisho. Jambo hilo

litatatiza ikiwa kipande cha sarufi kinachozingatiwa ni kimiliki pekee. Kwa mfano:

14)

[gombε	<u>w</u> angu]	/ <u>u</u> +angu/
[kondoo	<u>w</u> angu]	/ <u>u</u> +angu/
[bubu	<u>w</u> ako]	/ <u>u</u> +ako/
[kaḁi	<u>w</u> etu]	/ <u>u</u> +etu/

Katika mifano tuliyoitoa hapo juu, ni vigumu kutofautisha kama [gombε ; kondoo , bubu na kaḁi] yako katika hali ya uchache au wingi. Hii ni kwa sababu kila mojawapo ya vitu vilivyotajwa chaweza kumilikiwa na watu wengi au kwa hali ya wingi kimilikiwe na mtu mmoja.

Tukiangalia hali ambapo jina linalohusika huwa na kiambisho, tutaona kwamba wingi wadhihirika bila matatizo yo yote. Kwa mfano:

15)

[wazεε	<u>w</u> angu]	/ <u>u</u> +angu/	(baba na mama)
[vijana	<u>w</u> akε]	/ <u>u</u> +akε/	
[madaktari	<u>w</u> enu]	/ <u>u</u> +enu/	
[mafundi	<u>w</u> ao]	/ <u>u</u> +ao/	na kadhalika.

2.3.0 NGELI YA TATU

(Mofemu {mu} ndiyo kiambisho cha majina katika ngeli hii.)

Katika Kiswahili sanifu, ngeli ya tatu huwa na majina ya aina kadha. Kauli moja ya kijumla iwezayo kutolewa kuhusu ngeli hii ni kwamba (inayasheheni majina yote ya miti. Kwa mfano:

16)

[mnazi, msonobari, mbuni, mpera, mpingo
mtsungwa] na kadhalika.

Ngeli hiyo pia huwa na baadhi ya vitu vinavyotengenezwa kutoka sehemu za miti. Kwa mfano:

17)

[mkongolo, mkeka, msale, mkuki, mwiko], na kadhalika.

Ngeli ya tatu pia huwa na majina ya baadhi ya viungo vya mwili. Kwa mfano:

18)

[mkono, mguu, mdomo, mkia, msipa, mgongo]

Sifa inayodhihirika katika majina ya viungo vya mwili vilivyotajwa hapo juu ni kwamba ni virefu na

vyenye umbo la mviringo.

Aina nyingine ya majina yanayopatikana katika ngeli ya tatu ni ya vitu vya kimaumbile vinavyoenea.

Kwa mfano:

19)

[mto , mlima, msitu, mwinuko]

na kadhalika.

Ngeli ya tatu pia huwa na baadhi ya majina yanayoundwa kutokana na vitenzi. Majina hayo huundwa kwa kukitanguliza kiambisho cha ngeli kwenye shina la kitenzi. [a] inayotokea mwishoni mwa vitenzi vya lugha za Kibantu huondolewa na nafasi yake ikachukuliwa na { o } . Kwa mfano:

20)

[mlia]	kutokana na kitenzi	[lia]
[mtora]	kutokana na kitenzi	[tora]
[mgoma]	kutokana na kitenzi	[goma]
[mwangoza]	kutokana na kitenzi	[ngoza]
[mwamko]	kutokana na kitenzi	[amka]
[mwinuko]	kutokana na kitenzi	[inuka]
[mwanzo]	kutokana na kitenzi	[anza]

(Kuna aina ya majina ya kidhahania yanayopatikana katika ngeli ya tatu. Majina hayo yaonekana kuwa

yamekopwa kutoka Kiarabu. Kwa mfano:

21)

[muujiza, msikeli, mkataba] na
kadhalika.)

2.3.1 VIASHIRIA KATIKA NGELI YA 3

Majina huwakilishwa na mofemu {u} kwenye viashiria katika ngeli ya tatu iwapo ashirio ni la karibu na mtu anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. {o} hutumiwa kwa ashirio la karibu na anayesikiliza. Mofemu hizo, {u} na {o} hutumiwa kama virejeleo ikiwa kitu kinachotajwa chajulikana na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Kwa mfano:

22)

[mti	-	h <u>u</u>	hu <u>o</u>	<u>u</u> le]
[mkuki	-	h <u>u</u>	hu <u>o</u>	<u>u</u> le]
[mtu	-	h <u>u</u>	hu <u>o</u>	<u>u</u> le]
[mwinuko	-	h <u>u</u>	hu <u>o</u>	<u>u</u> le]
[mwongozo	-	h <u>u</u>	hu <u>o</u>	<u>u</u> le]
[mwanzo	-	h <u>u</u>	hu <u>o</u>	<u>u</u> le]

2.3.2 SIFA KATIKA NGELI YA 3

(Kiambisho kinachowakilisha jina kwenye sifa katika ngeli hii ni {mu} . Kwa mfano:

23)

[mkuki	<u>mr</u> ɛfu]	/ <u>mu</u> +rɛfu /)
[mti	<u>m</u> wɛbamba]	/ <u>mu</u> +ɛbamba /)
[msitu	<u>m</u> kubwa]	/ <u>mu</u> +kubwa /
[mtɔɛ zɔ	<u>m</u> zuri]	/ <u>mu</u> +zuri /
[mliɔ	<u>m</u> baja]	/ <u>mu</u> +baja /
[mtɔ	<u>m</u> pana]	/ <u>mu</u> +pana /

2.3.3 VITENZI KATIKA NGELI YA 3

(Kiwakilishi cha jina kwenye vitenzi katika ngeli ya tatu ni mofemu {u} . Kwa mfano:

24)

[mti	<u>u</u> lianguka]
[mkuki	<u>u</u> mɛtupwa]
[mtɔ	<u>u</u> tafurika])
[msitu	<u>u</u> mɛtɔmɛka]
[mtɔɛ zɔ	<u>u</u> taanza]
[mliɔ	<u>u</u> nasikika]

2.3.4 KIJINA KIHUSISHI CHA NGELI YA 3

(Mofemu {o} ndiyo itumiwayo kama kijina kihusishi cha majina katika ngeli ya tatu. Kwa mfano:

25)

[mtaro]	ulio <u>t</u> simbwa]
[mkono]	ulio <u>k</u> atwa])
[mto]	ulio <u>f</u> urika]
[msitu]	una <u>a</u> tomeka]
[mtεzo]	ulio <u>a</u> anza]
[mlio]	utaka <u>s</u> sikika]

2.3.5 IDADI KATIKA NGELI YA 3

(Katika ngeli hii, majina huwakilishwa na mofemu {m} kwenye kipande cha idadi. Kwa mfano:

26)

[mti]	<u>m</u> moja]
[mguu]	<u>m</u> moja])
[mto]	<u>m</u> moja]
[mkuki]	<u>m</u> moja]
[mkaka]	<u>m</u> moja]
[mtεzo]	<u>m</u> moja]

2.3.6 VIMILIKI KATIKA NGELI YA 3

(Mofemu {u} ndiyo inayotumiwa kama kiwakilishi cha jina kwenye vimiliki vya ngeli ya tatu. Kwa mfano:-

27)

[mti	wangu]	/u+angu/
[mkuki	wako]	/u+ako/)
[mlio	wake]	/u+ake/
[mto	wetu]	/u+etu/
[mt)ezo	wenu]	/u+enu/
[mpango	wao]	/u+ao/ *

2.4.0 NGELI YA NNE

(Ngeli hii huyasheheni majina yaliyo wingi wa yale yanayopatikana katika ngeli ya tatu. Mofemu {mi} ndiyo inayotumika kama kiambisho cha jina katika ngeli ya nne.

Kuna aina ya majina katika ngeli ya nne ambayo hayawezi kutokea katika hali ya umoja (uchache).

[mi-] inayotokea kwenye mianza ya majina hayo ni sehemu ya shina; si kiambisho. Majina hayo ni kama vile [miwani] na [miadi].

2.4.1 VIASHIRIA KATIKA NGELI YA 4

(Mofemu {i} hutumiwa kwa kuyawakilisha majina kwenye viashiria katika ngeli hii iwapo ashirio ni la karibu na mtu anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Mofemu {jo} hutumia kuashiria vitu vilivyo karibu na anayesikiliza. Mofemu hizo pia hutumiwa kurejelea vitu vinavyojulikana kwa mtu anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Kwa mfano:

28)

[miti -	hii	hijɔ	ilɛ])
[mikuki -	hii	hijɔ	ilɛ]) .
[mikatɛ -	hii	hijɔ	ilɛ]
[misitu -	hii	hijɔ	ilɛ]
[mitɛzo -	hii	hijɔ	ilɛ]
[miliɔ -	hii	hijɔ	ilɛ]

2.4.2 SIFA KATIKA NGELI YA 4

(Majina ya ngeli ya nne huwakilishwa na mofemu {mi} kwenye kipande cha sifa. Kwa mfano:

29)

[miti	<u>mirɛfu</u>])
[miwani	<u>mizuri</u>]
[miadi	<u>mibaja</u>]
[mito	<u>mipana</u>]
[mikuki	<u>mifupi</u>]
[misitu	<u>mikubwa</u>]

2.4.3 VITENZI KATIKA NGELI YA 4

(Mofemu {i} ndiyo inayotumiwa kama kiwakilishi cha majina kwenye (^{vitenzi}kipande cha idadi) katika ngeli hii.

Kwa mfano:

30)

[miti	<u>ilikatwa</u>]
[miwani	<u>imɛvunjika</u>])
[miadi	<u>itatimizwa</u>]
[mito	<u>imɛfurika</u>]
[mikuki	<u>inalɛtwa</u>]
[misitu	<u>ilitɔmɛka</u>]

2.4.4 KIJINA KIHUSISHI KATIKA NGELI YA 4

(Mofemu {jo} hutumiwa kama kijina kihusishi katika ngeli ya nne. Kwa mfano:-

31)

[miti	ilij _o katwa]
[miwani	inaj _o vun _g ika]
[miadi	itakaj _o timizwa]
[mit _o	itakaj _o furika]
[mikuki	inaj _o l _e twa]
[misitu	ilij _o t _o meka]

2.4.5 IDADI KATIKA NGELI YA 4

(Majina huwakilishwa kwenye idadi na mofemu {mi} katika ngeli ya nne. Mofemu hiyo huwepo tu iwapo kiasi kinachotajwa ni mbili, tatu, nne, tano na nane. Kiwakilishi cha jina huwa hakipo ikiwa idadi inayotajwa ni sita, saba, tisa au kumi). Kwa ujumla tungesema kwamba mofemu {mi} na alomofu yake ambayo ni kapa ndizo zinazotumiwa kuyawakilisha majina kwenye idadi yo yote ile katika ngeli ya nne. Kwa mfano:-

32)

([miti	miwili]
[mit _o	mitatu]
[mikuki	minne]
([milima	sita]
[mikong _o jo	saba]
[mits _o zo	kumi]

2.4.6 VIMILIKI KATIKA NGELI YA 4

(Mofemu {i} hutumiwa kuyawakilisha majina kwenye vimiliki katika ngeli hii) Sauti [j] inayotokea kwenye vimiliki katika maandishi husababishwa na sheria ya kifonetiki. Kulingana na sheria hiyo, vokali [i] hugeuka na kuwa nusu vokali au kiyeyusho [j] ikiwa imeitangulia vokali nyingine yo yote ile isipokuwa i .

SHERIA "D"

i → j / - v⁵

Ifuatayo ni mifano inayoonyesha jinsi majina ya ngeli ya nne yanavyochukuana na vimiliki.

33)

[miwani	ɟangu]	/ i+angu /
[mitɕɛ zɔ	ɟɛtu]	/ i+ɛtʉ / ɔ
[miguu	ɟakɔ]	/ i+akɔ / •
[miadi	ɟakɛ]	/ i+akɛ /
[mikɔngɔɔ	ɟɛnu]	/ i+ɛnu /
[mifuko	ɟaɔ]	/ i+aɔ /

2.5.0 NGELI YA TANO . *

(Kiambisho cha jina katika ngeli hii huwa mofemu {ji} iwapo shina la jina lina silabi moja pekee) Kiambisho cha jina hakipo kwenye majina yaliyo na mashina yenye silabi zaidi ya moja.

Chambilecho Loogman (1965:28), mashina yaliyo na kiambisho {ji} ni machache sana ingawa wanasarufi wanaoutumia mpangilio wa ngeli unaozingatia viambisho huiita ngeli ya tano "ji". Kauli aliyoitoa Loogman ni kwamba idadi ya majina yaliyo na kiambisho {ji} ni takribani ishirini na matano.

(Ngeli ya tano huyasheheni majina yaliyo na misingi tofauti kimaana. Kwa mfano:-

- (a) Baadhi ya majina ya viungo vya mwili kama vile:-

34)

[sikiɔ ; bɛga, gɔti, jitiɔ ; jino]

Polome (1967:97); Ashton (1947:65) na Mbaabu (1978:37) ni baadhi ya wanasarufi wanaoshikilia kwamba majina ya sehemu za mwili yaliyotolewa hapo juu yana sifa moja maalum. Kauli yao ni kwamba viungo hivyo hutokea yiwili viwili (jozi). [mguu] na [mkono] ni viungo vinavyotokea yiwili yiwili

lakini haviko katika ngeli ya tano. Kwa hivyo inatubidi kuitilia shaka kauli ya wanasarufi tuliowataja hapo awali (Polome, Ashton na Mbaabu).

Sifa ya ujumla tuliyoiona kati ya majina ya viungo vya mwili vilivyo katika ngeli ya tano ni kwamba (umbo lao la nje ni la mviringo au linalokaribia mviringo.)

(b) Aina nyingine ya majina yanayopatikana katika ngeli hii huwa yaonyesha (hali ya ukubwa wa majina kutoka ngeli tofauti.

Kwa mfano:-

35)

[jisu]	ukubwa wa	[kisu]	(ngeli ya 7)
[jibwa]	ukubwa wa	[mbwa]	(ngeli ya 1)
[jumba]	ukubwa wa	[pumba]	(ngeli ya 9)
[jiti]	ukubwa wa	[mti]	(ngeli ya 3)

(c) Ngeli ya tano pia (huwa na baadhi ya majina yaliyoundwa kutokana na vitenzi. Kwa mfano:⁶

36)

[pigɔ]	kutokana na kitenzi	[piga]
[nɛnɔ]	kutokana na kitenzi	[nɛna]
[ɔɔɔ]	kutokana na kitenzi	[ɔɔa]

[tatizɔ] kutokana na kitenzi [tatiza]

[patɔ] kutokana na kitenzi [pata]

[tungɔ] kutokana na kitenzi [tunga]

(d) (Kuna baadhi ya majina ya sehemu za miti ambayo hupatikana katika ngeli hii. Kwa mfano:

[tunda, Sina
ua , tawi
jani , ganda])

2.5.1 VIASHIRIA KATIKA NGELI YA 5

(Mofemu {li} | hutumiwa kama |kiwakilishi cha jina kwenye viashiria) katika ngeli hii (iwapo kitu kinachoashiriwa kiko karibu na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Vile vile mofemu {li} inatumiwa kwa ashirio la mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Mofemu {lɔ} hutumiwa ikiwa ashirio ni la karibu na mtu anayesikiliza.

Mofemu {li} na {lɔ} pia hutumiwa kama virejeleo ikiwa kitu kinachotajwa chajulikana kwa anayezungumza pamoja na anayesikiliza.

37)

[jiwε	—	hili	hilɔ	lilε]
[jumba	—	hili	hilɔ	lilε])
[sanduku	—	hili	hilɔ	lilε]
[sikiɔ	—	hili	hilɔ	lilε]
[tunda	—	hili	hilɔ	lilε]
ʒɔɔ	—	hili	hilɔ	lilε]

2.5.2 SIFA KATIKA NGELI YA 5

Katika ngeli hii, majina hayawakilishwi na kiambisho cho chote kwenye sifa. Nafasi ya kiambisho huwa kapa {∅} . Kwa mfano:-

38)

[jumba	kubwa]
[jibwa	kali]
[jina	zuri]
[Samba	pana]
[tiɔ	kubwa]
[tunda	tamu]

[ɣoto]	"sikio"	[koɣoro]	"mguu"
[ɣwɔkɔ]	"mkono"		

Majina hayo matatu huwa na wingi wake katika ngeli ya sita. Kwa mfano:

242)

wingi wa	[ɣoto]	"sikio"	ni	[mato]	"masikio"
wingi wa	[koɣoro]	"mguu"	ni	[maɣoro]	"miguu"
wingi wa	[ɣwɔkɔ]	"mkono"	ni	[mɔkɔ]	/ma+ɔkɔ/ "mikono"

(b) Aina nyingine ya majina yapatikanayo katika ngeli ya kumi na tano huwa yameundwa kutokana na vitenzi.

Majina hayo huundwa kwa kuitanguliza mofemu

{ko} kwenye mianzo ya vitenzi. Kwa mfano:

243)

[<u>ko</u> rera]	"kulia" kutokana na [rera]	"lia"
[<u>ko</u> rema]	"kulima" kutokana na [rema]	"lima"
[<u>ko</u> ḡma]	/ <u>ko</u> +ḡma/ "kusoma" kutokana na [ḡma]	"soma"
[<u>ko</u> ɛra]	"kulea" kutokana na [ɛra]	"lea"
[<u>ko</u> hora]	"kupiga" kutokana na [hora]	"piga"
[<u>ko</u> ɛhɛ]	"kuleta" kutokana na [ɛhɛ]	"leta"
[<u>ko</u> ḡɛka]	/ <u>ko</u> +ḡɛka/ "kucheka" kutokana na [ḡɛka]	"cheka"

na kadhalika.

3.15.1 VIASHIRIA KATIKA NGELI YA 15

Katika ngeli hii, majina huwakilishwa na mofemu {ko} kwenye viashiria. Mofemu hiyo pia hutumika kama kirejeleo iwapo kitu kinachotajwa chafahamika kwa mtu anayezungumza pamoja na yule anayesikiliza.

Mofemu {ko} aghalabu hutumika kama kirejeleo kuliko kiashiria ikiwa jina linalohusika limeundwa kutokana na kitenzi. Hii ni kwa sababu majina ya aina hiyo ni ya kidhahania.

Ifuatayo ni mifano ionyeshayo jinsi majina ya ngeli ya kumi na tano yanavyochukuana na viashiria.

tfi tja

244)

- [koɣoro ɣoko /koko/ kou ko:rea]
- [ɣwoko ɣoko /koko/ kou ko:rea]
- [ɣoto ɣoko /koko/ kou ko:rea]

3.15.2 SIFA KATIKA NGELI YA 15

Majina ya ngeli hii huwakilishwa na mofemu

{ko} kwenye kipande cha sifa. Kwa mfano:

245)

- [ɣwoko koraihu] "mkono mrefu"
- [koɣoro ɣoɖeke] /koɖeke/ "mguu mwebamba"
- [ɣoto konini] "sikio dogo"
- [korera ko:ru] "kulia kubaya"
- [ɣoɖeka kwɛɣa] /ko+ɛɣa/ "kucheka kuzuri"

3.15.3 VITENZI KATIKA NGELI YA 15

Katika ngeli hii, mofemu {ko} ndiyo inayoyawakilisha majina kwenye vitenzi. Kwa mfano:

246)

- ^{kijurū} [koɣoro ne koimbu] "mguu umevimba" 0
- [ɣwoko ne koratɛmirwɔ] "mkono ulikatwa"
- [ɣoto ne kohɔnu] "sikio limepona"
- [korera ɣotjetekeretɔ] "kulia hakukubaliwi"
- [korema ne kwɛndɛtwɔ] /ko+ɛndɛtwɔ/ "kulima kunapendwa"

ū 0

3.15.4 KIJINA KIHUSISHI KATIKA NGELI YA 15

Mofemu {ko} ndiyo itumiwayo kama kijina
kihusishi katika ngeli hii. Kwa mfano:

247)

[χwɔkɔ korea koratɛmirwɔ] "mkono uliokatwa"

[koɣoro korea koimbu] "mguu uliovimba"

[χoto korea kohɔnu] "sikio lililopona"

[korema korea kwɛndɛtwɔ] /ko+ɛndɛtwɔ / "kulima kunakopendw"

[χɔɛka korea koɣirjɛ] "kucheka kulikokatazwa"

[korɔɣama korea χotarahɔtɛka] /kotarahɔtɛka/ "kusimama

kusikowezezana"

3.15.5 IDADI KATIKA NGELI YA 15

Katika ngeli hii, mofemu {ko} ndiyo inayotumiwa
ili kuyawakilisha majina kwenye kipande cha idadi.

Majina ya sehemu za mwili yaliyoko katika ngeli
hii ndiyo tu yanayoweza kuhesabiwa. Kwa mfano:

248)

[χwɔkɔ komwɛ] "mkono mmoja"

[koɣoro komwɛ] "mguu mmoja"

[χoto komwɛ] "sikio moja"

3.15.6 VIMILIKI KATIKA NGELI YA 15

Mofemu {ko} ndiyo inayoyawakilisha majina
kwenye vimiliki katika ngeli hii. Kwa mfano:

249)

[koɣoro	ɣwakwa]	/ko+akwa/	"mguu wangu"
[ɣwɔkɔ	ɣwaku]	/ko+aku/	"mkono wako"
[ɣoto	ɣwake]	/ko+akɛ/	"sikio lake"
[ɣoɕaka	ɣwito]	/ko+ito/	"kucheza kwetu"
[korakara	kwaju]	/ko+aju/	"kukasirika kwenu"
[koruɣa	kwao]	/ko+ao/	"kupika kwao"

3.16.0 NGELI YA KUMI NA SITA

Ngeli hii huwa na jina moja pekee. Jina hilo ni [hando] "pahali" na hutumiwa katika kuonyesha sehemu ambayo haijaenea. Yaani sehemu halisi.

Kiambisho cha jina katika ngeli ya kumi na sita ni mofemu {ha} .

3.16.1 VIASHIRIA KATIKA NGELI YA 16

Katika ngeli hii, jina huwakilishwa na mofemu {ha} kwenye viashiria. Mofemu hiyo pia hutumiwa kama kirejeleo ikiwa pahali panapotajwa pafahamika kwa mtu anayezungumza pamoja na yule anayesikiliza. Kwa mfano:

250)

[hando - haha hau ha:rea]

3.16.2 SIFA KATIKA NGELI YA 16

Katika ngeli hii, mofemu {ha} hutumiwa ili kuliwakilisha jina kwenye kipande cha sifa. Kwa mfano:

251)

[hando	<u>ha</u> ʒεkε]	"pahali pebamba"
[hando	<u>hε</u> :ʒa] /ha+εʒa/	"pahali pazuri"
[hando	<u>hɔ</u> :ru] /ha+ɔru/	"pahali pabaya"
[hando	<u>har</u> aihu]	"pahali parefu"
[hando	<u>han</u> ini]	"pahali padogo"
[hando	<u>haj</u> ge]	"pahali pengine"

3.16.3 VITENZI KATIKA NGELI YA 16

Mofemu {ha} hutumiwa ili kuliwakilisha jina kwenye vitenzi katika ngeli hii. Kwa mfano:

252)

[hando	ne	<u>hah</u> atirwɔ]	"pahali palifagiwa"
[hando	ne	<u>hax</u> akwɔ]	"pahali patajengwa"
[hando	ne	<u>hare</u> mε]	"pahali pamelimwa"
[hando	ne	<u>hara</u> ʔɔndεkirwɔ]	"pahali palitengenezwa"
[hando	ne	<u>haxa</u> ʔamerwɔ]	"pahali patahamiwa"
[hando	ne	<u>hε</u> :ndε]/ha+εndε/	"pahali papendwa"

3.16.4 KIJINA KIHUSISHI KATIKA NGELI YA 16

Katika ngeli hii, mofemu {ha} ndiyo itumiwayo kama kijina kihusishi. Kwa mfano:

253)

[hando	<u>h</u> area	<u>haha</u> tirwo]	"pahali palipofagiwa"
[hando	<u>h</u> area	<u>hara</u> ɔndɛkirwo]	"pahali palipotengenezwa"
[hando	<u>h</u> area	<u>hak</u> aremwo]	"pahali patakapolimwa"
[hando	<u>h</u> area	<u>hax</u> akwo]	"pahali patakapojengwa"
[hando	<u>h</u> area	<u>hɛ:ndɛ</u> /ha+ɛndɛ/	"pahali panapopendwa"
[hando	<u>h</u> area	<u>hara</u> ɔamirwo]	"pahali palipohamwa"

3.16.5 IDADI KATIKA NGELI YA 16

Mofemu {ha} ndiyo inayotumiwi ili kuliwakilisha jina kwenye kipande cha idadi katika ngeli hii. Kwa mfano:

254)

[hando	<u>h</u> amwe]	"pahali pamoja"
--------	----------------	-----------------

3.16.6 VIMILIKI KATIKA NGELI YA 16

Katika ngeli hii, mofemu {ha} ndiyo inayoliwakilisha jina kwenye vimiliki. Kwa mfano:

255)

[hando	<u>h</u> akwa]	"pahali pako"
[hando	<u>h</u> aku]	"pahali pako"
[hando	<u>h</u> akɛ]	"pahali pake"
[hando	<u>h</u> aito]	"pahali petu"
[hando	<u>h</u> apu]	"pahali penu"
[hando	<u>h</u> a:ɔ]	"pahali pao"

3.17.0 NGELI YA KUMI NA SABA

Ngeli hii ina jina moja pekee ambalo ni [kondo] "mahali". Jina hilo hutumiwa ili kumaanisha mahali kwa jumla. Yaani ni kinyume cha ngeli ya kumi na sita.

Kiambisho cha jina katika ngeli ya kumi na saba ni mofemu {ko} ambayo hukaririwa kwenye vipande vingine vya sarufi kama tutakavyodhibitisha hapo baadaye.

3.17.1 VIASHIRIA KATIKA NGELI YA 17

Katika ngeli hii mofemu {ko} ndiyo inayotumiwa ili kuliwakilisha jina kwenye viashiria. Mofemu hiyo pia hutumiwa kama kirejeleo iwapo mahali kunakohusika kwajulikana kwa mtu anayezungumza pamoja na yule anayesikiliza. Kwa mfano:

256)

[kondo] yoko / koko / kou ko:rea]

3.17.2 SIFA KATIKA NGELI YA 17

Mofemu {ko} ndiyo itumiwayo ili kuliwakilisha jina kwenye kipande cha sifa. Kwa mfano:

257)

[kondo kwεga] /ko+εga/ "mahali kuzuri"

[kondo ko:ru] "mahali kubaya"

[kondo χoδeru] /koδeru/ "mahali safi"

[kondo koŋge] "mahali kwingine"

3.17.3. VITENZI KATIKA NGELI YA 17

Katika ngeli hii, mofemu {ko} ndiyo inayotumiwa ili kuliwakilisha jina kwenye vitenzi. Kwa mfano:

258)

[kondo	ne	<u>koreme</u>]	"mahali kumelinwa"
[kondo	ne	<u>γoðame</u>]	"mahali kumehanwa"
[kondo	ne	<u>korahatirwo</u>]	"mahali kulifagiwa"
[kondo	ne	<u>korakirwo</u>]	"mahali kulijengwa"
[kondo	ne	<u>korahja</u>]	"mahali kunachomeka"

3.17.4 KIJINA KIHUSISHI KATIKA NGELI YA 17

Mofemu {ko} hutumiwa kama kijina kihusishi katika ngeli hii. Kwa mfano.

259)

[kondo	<u>korea</u>	<u>koreme</u>]	"mahali kulikolimwa"
[kondo	<u>korea</u>	<u>korakwo</u>]	"mahali kunakojengwa"
[kondo	<u>korea</u>	<u>korahja</u>]	"mahali kunakoçhomeka"
[kondo	<u>korea</u>	<u>kwahatwo</u>]/ko+ahatwo/	"mahali kulikofagiwa"

3.17.5 IDADI KATIKA NGELI YA 17

Katika ngeli hii, jina huwakilishwa na mofemu {ko} kwenye kipande cha idadi. Kwa mfano:

260)

[kondo	<u>komwe</u>]	"mahali kumoja"
[kondo	<u>koinge</u>]	"mahali kwingi"

3.17.6 VIMILIKI KATIKA NGELI YA 17

Katika ngeli hii mofemu {ko} hutumiwa ili kuliwakilisha jina kwenye vimiliki. Kwa mfano:

261)

[kondo	<u>ɣ</u> wakwa]	/ <u>ko</u> +akwa/	"mahali kwangu"
[kondo	<u>ɣ</u> waku]	/ <u>ko</u> +aku/	"mahali kwake"
[kondo	<u>ɣ</u> wakɛ]	/ <u>ko</u> +akɛ/	"mahali kwake"
[kondo	<u>ɣ</u> wito]	/ <u>ko</u> +ito/	"mahali kwetu"
[kondo	<u>kw</u> aju]	/ko+aju/	"mahali kwenu"
[kondo	<u>kw</u> aɔ]	/ko+aɔ/	"mahali kwao"

TANBIHI

1. Katika lugha ya Kikikuyu, [pipi] ina maana mbili. Maana ya kwanza ni udogo wa kimo, na ya pili ni uchache wa idadi. Katika muktadha wetu, tunaizingatia maana ya pili (uchache wa idadi)
2. Vokali [i] iliyoko mwanzoni mwa jina [ikomi] "kumi" ni sehemu ya shina sio kiambisho cha ngeli.
3. Rejelea Sheria "E"

SURA YA NNE

4.0.0 ULINGANISHI WA NGELI ZA KISWAHILI NA
ZA KIKIKUYU

4.1.0 UTANGULIZI

Kiswahili na Kikikuyu ni lugha za nasaba moja. Zote ni lugha za Kibantu. Kwa hivyo lugha hizo hazina budi kuwa na ulinganifu fulani katika viwango vya muundo na maana. Vile, vile, kila mojawapo ya lugha hizo haina budi kuwa na sifa maalum ambazo zinaitambulisha.

Katika sura hii tutazilinganisha lugha mbili tunazozishughulikia ili tuone zinavyofanana na kutofautiana. Ulinganishi wetu utazingatia mambo matatu muhimu. Mambo hayo ni: idadi za ngeli, wiano wa kisarufi, na misingi ya kimaana inayotokea katika ngeli za lugha hizo, Kiswahili sanifu na Kikikuyu.

4.1.1 IDADI ZA NGELI

Katika Kiswahili sanifu, kuna jumla ya ngeli kumi na sita. Ngeli hizo ni moja hadi kumi na moja, na pia kumi na nne hadi kumi na nane. Kwa hivyo ngeli ya kumi na mbili na kumi na tatu hazimo katika Kiswahili sanifu.

Kikikuyu kina jumla ya ngeli kumi na saba. Ngeli hizo zinafululiza kuanzia ya kwanza hadi ya kumi na saba.

4.1.2 WIANO WA KISARUFI

Ngeli za Kiswahili na za Kikikuyu zinatofautiana sana katika kiwango cha viambisho vya majina na mofemu zinazoyawakilisha majina kwenye vipande vingine vya sarufi.

Ngeli za sita, tisa, na kumi zina viambisho vinavyofanana katika lugha zote mbili. Kiambisho cha ngeli ya sita ni {ma} ; Baadhi ya majina ya ngeli ya tisa yana kiambisho {n} na mengine hayana. Kiambisho cha jina katika ngeli ya kumi ni sawa na cha ngeli ya tisa. Yaani {n} kwenye baadhi ya majina na kapa {∅} kwenye baadhi ya majina mengine.

Majina ya ngeli ya kwanza katika Kiswahili yana viambisho tofauti. Kunayo yenye {mu} kama vile [mtu, mzeεε , mwalimu] ; mengine yana {ki} kwa mfano [kijana, kiwεtε] na kadhalika. Kuna mengine yenye kiambisho {n} kama vile [nzigε , mbu] , na pia kuna mengine ambapo nafasi ya kiambisho ni kapa {∅} kwa mfano [kondoo , kaḁi, bubu] na kadhalika.

Ingawa majina ya ngeli ya kwanza katika Kiswahili yana viambisho vinavyotofautiana, mofemu zinazoyawakilisha kwenye vipande vingine vya sarufi ni sawa. Ashirio la karibu na anayezungumza ni {ju} nalo la karibu na anayesikiliza ni {jo} . Kiwakilishi cha majina hayo kwenye sifa ni {mu} , na kwenye kitenzi

ni {a} , kijina kihusishi ni {jε} ; kwenye idadi ni {mυ} , na kwenye vimiliki ni {u} .

Majina ya ngeli ya kwanza katika Kikikuyu yana kiambisho {mo} . Majina hayo huwakilishwa na mofemu {o} kwenye viashiria, {mo} kwenye sifa, {a} kwenye vitenzi, na {o} kwenye kijina kihusishi, idadi pamoja na vimiliki.

Katika Kiswahili, ngeli ya pili huwa na majina yenye viambisho vinavyotofautiana. Kuna yaliyo na {wa} , kama vile [watoto , wazee , walimu] ; mengine yana {vi} . Kwa mfano [vijana, viwete , vipofu] . Hali kadhalika kunayo yenye kiambisho {ma} . Kwa mfano [makarani, mafundi] . Ngeli hiyo pia huwa na majina yasiyo na viambisho. Kwa mfano [kadi, kandoo, fundi] , na kadhalika.

Majina ya ngeli ya pili katika Kiswahili huwakilishwa na mofemu {wa} kwenye viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na yule anayesikiliza. Mofemu hiyo pia huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye sifa, vitenzi na idadi. {o} ndiyo mofemu inayoyawakilisha majina kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumika kama kijina kihusishi.

Katika Kikikuyu, majina ya ngeli ya pili huwa na kiambisho {a} . Kiambisho hicho pia huyawakilisha

majina ya ngeli hiyo kwenye viashiria, sifa, idadi na vimiliki. Mofemu {ma} huyawakilisha kwenye vitenzi.

Katika Kiswahili sanifu, mofemu {ru} ndiyo kiambisho cha majina ya ngeli ya tatu. Mofemu hiyo pia hutokea kwenye vipande vya sifa na idadi. Mofemu {u} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye viashirio vya karibu na mtu anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na yule anayesikiliza. Aidha, mofemu {u} hutokea kwenye vitenzi na vimiliki. Mofemu huyawakilisha majina ya ngeli ya tatu kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumika kama kijina kihusishi.

Katika Kikikuyu, majina ya ngeli ya tatu huwa na kiambisho {mo} ambacho pia hutokea kwenye kipande cha sifa. Mofemu {o} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye viashiria, vitenzi, kijina kihusishi, idadi, na vimiliki.

Katika Kiswahili, ngeli ya nne huwa na majina yenye kiambisho {mi} ambacho pia hutokea kwenye sifa na idadi. Mofemu {i} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye viashiria, vitenzi na vimiliki. {jo} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumika kama kijina kihusishi.

Ngeli ya nne katika Kikikuyu huwa na majina yenye kiambisho {me} . Kiambisho hicho pia hutokea kwenye kipande cha sifa. Majina hayo huwakilishwa na mofemu {e} kwenye viashiria, vitenzi, kijina kihusishi, idadi, na pia vimiliki.

Katika Kiswahili, majina mengi ya ngeli ya tano aghalabu huwa hayana viambisho. Ni majina machache tu yaliyo na kiambisho {i} . Mofemu hiyo haitokei kwenye kipande kingine chochote cha sarufi. Majina ya ngeli hiyo huwakilisha na mofemu {li} kwenye viashirio vya karibu na anayesikiliza au mbali na anayezungunza pamoja na anayesikiliza. Mofemu hiyo pia hutokea kwenye vitenzi. Mofemu {lo} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumiwa kama kijina kihusishi. Mofemu {la} huyawakilisha majina hayo kwenye vimiliki.

Majina ya ngeli ya tano katika Kikikuyu huwa na kiambisho {re} na mengine huwa na {i} . Mofemu {re} ndiyo inayotawala wiano wa kisarufi kwa sababu hukaririwa kwenye vipande vingine vyote. Yaani viashiria, sifa, vitenzi, kijina kihusishi, idadi, na vimiliki. Mofemu {i} huyawakilisha majina yenye kiambisho {i} kwenye kipande cha sifa.

Katika Kiswahili, ngeli ya sita huwa na majina

yenye kiambisho {ma} ambayo pia hutokea kwenye vipande vya sifa na idadi. Mofemu {ja} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na yule anayesikiliza. Mofemu hiyo pia hutokea kwenye vitenzi. Mofemu {jo} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutuniwa kama kijina kihusishi. Mofemu {i} huyawakilisha majina ya ngeli ya sita kwenye vimiliki.

Ngeli ya sita katika Kikikuyu huwa na majina yenye kiambisho sawa na kile kinachopatikana katika Kiswahili. Yaani {ma}. Lakini katika Kikikuyu, kiambisho cha majina hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi.

Katika Kiswahili, ngeli ya saba huwa na majina yenye kiambisho {ki}. Mofemu hiyo hukaririwa kwenye vipande vingine vyote.

Kiambisho cha majina ya ngeli ya saba katika Kikikuyu ni mofemu {ke}. Mofemu hiyo pia hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi.

Katika Kiswahili, majina ya ngeli ya nane huwa na kiambisho {vi} ambacho pia hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi. Yaani viashiria, sifa, vitenzi, kijina kihusishi, idadi na vimiliki.

Kiambisho cha majina ya ngeli ya nane katika Kikikuyu ni mofemu {i} . Mofemu hiyo pia hutokea kwenye viashiria, vitenzi, kijina kihusishi, na idadi. Kiwakilishi cha majina hayo kwenye kipande cha sifa ni mofemu {n} ambayo hutokea tu kwenye mashina yanayoanza kwa sauti zenye msepetuko. Mofemu {i} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye vimiliki.

Katika Kiswahili, ni baadhi tu ya majina ya ngeli ya tisa ambayo huwa na kiambisho {n} . Nafasi ya kiambisho kwenye mengi ya majina ya ngeli hiyo huwa kapa. Kiambisho {n} pia hutokea kwenye kipande cha sifa. Mofemu {i} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye viashiria, vitenzi, kijina kihusishi, na vimiliki. Majina hayo hayawakilishwi na mofemu yoyote kwenye kipande cha idadi.

Kama tulivyodokeza hapo awali, majina ya ngeli ya tisa katika Kikikuyu huwa na umbo unaofanana na yale yanayopatikana kwenye ngeli hiyo katika Kiswahili. Yaani kiambisho ni {n} au {Ø} . Pia mofemu {n} hutokea kwenye baadhi ya sifa. Mofemu {e} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye viashiria, vitenzi, kijina kihusishi, idadi, na pia vimiliki.

Katika Kiswahili pamoja na Kikikuyu, ngeli ya kumi huwa na majina yenye umbo sawa na ya ngeli

ya tisa. Pia kuna kufanana katika kipande cha sifa ambapo {n} hutokea kwenye baadhi ya sifa au nafasi ya kiambisho huwa kapa.

Tofauti baina ya ngeli ya kumi katika Kiswahili na ngeli hiyo katika Kikikuyu hutokea kwenye vipande vingine vya sarufi. Kwa mfano.

Katika Kiswahili, majina ya ngeli ya kumi huwakilishwa na mofemu {zi} kwenye vitenzi na pia viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na yule anayesikiliza. Mofemu {zo} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumiwa kama kijina kihusishi. Mofemu {za} huyawakilisha majina hayo kwenye vimiliki.

Katika Kikikuyu, majina ya ngeli ya kumi huwakilishwa na mofemu {i} kwenye viashiria, vitenzi, kijina kihusishi, na idadi. Mofemu {si} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye vimiliki.

Katika Kiswahili, ngeli ya kumi na moja huwa na majina yenye kiambisho {u} ambacho hukaririwa kwenye viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Mofemu hiyo pia hutokea kwenye vitenzi na vimiliki. Mofemu {o} huyawakilisha majina hayo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumiwa kama kijina

kihusishi.

Majina ya ngeli ya kumi na moja katika Kikikuyu huwa na kiambisho {ro} . Kiambisho hicho hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi.

Ngeli za kumi na mbili na kumi na tatu zapatikana tu katika Kikikuyu. Hazipo katika Kiswahili. Kiambisho cha majina ya ngeli ya kumi na mbili ni {ka} na hukaririwa kwenye vipande vingine vyote.

Katika ngeli ya kumi na tatu, majina huwa na kiambisho {to} . Kiambisho hicho pia hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi.

Katika Kiswahili, ngeli ya kumi na nne huwa na majina yenye kiambisho sawa na ngeli ya kumi na moja. Yaani {u} . Kiambisho hicho vilevile hukaririwa kwenye vitenzi, vimiliki, na viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Mofemu {o} huyawakilisha majina ya ngeli hiyo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza, na pia hutumiwa kama kijina kihusishi. Mofemu {mu} huyawakilisha majina hayo kwenye kipande cha sifa. Majina ya ngeli ya kumi na nne hayawakilishwi na mofemu yoyote kwenye kipande cha idadi. Kwa hivyo kimuundo, hiyo ndiyo tofauti ya kipekee iliyoko baina ya ngeli ya kumi na moja na kumi na nne.

Ngeli ya kumi na nne katika Kikikuyu huwa na majina yenye kiambisho {o} . Kiambisho hicho hukaririwa kwenye viashiria, vitenzi, idadi, vimiliki, na pia hutumiwa kama kijina kihusishi. Majina hayo huwakilishwa na mofemu {mo} kwenye kipande cha sifa.

Katika Kiswahili, majina ya ngeli ya kumi na tano huwa na kiambisho {ku} ambacho hukaririwa kwenye sifa, vitenzi, vimiliki, na pia kwenye viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Mofemu {ko} huyawakilisha majina hayo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumiwa kama kijina kihusishi. Majina ya ngeli hiyo hayawakilishwi kwenye kipande cha idadi.

Majina ya ngeli ya kumi na tano katika Kikikuyu huwa na kiambisho {ko} . Kiambisho hicho hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi.

Katika Kiswahili, ngeli ya kumi na sita huwa na jina lenye kiambisho {pa} . Kiambisho hicho hukaririwa kwenye sifa, vitenzi, idadi, vimiliki, na pia kwenye viashirio vya karibu na mtu anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Mofemu {po} huliwakilisha jina hilo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumiwa kama kijina kihusishi.

Ngeli ya kumi na sita katika Kikikuyu ina jina lenye kiambisho {ha} ambacho hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi.

Katika Kiswahili, ngeli ya kumi na saba huwa na kiambisho {ma} ambacho hakitokei kwenye kipande kingine. Mofemu {ku} huliwakilisha jina la ngeli hiyo kwenye sifa, vitenzi, idadi, vimiliki, na viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Nayo mofemu {ko} huliwakilisha jina la ngeli hiyo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumiwa kama kijina kihusishi.

Jina la ngeli ya kumi na saba katika Kikikuyu huwa na kiambisho {ko}. Kiambisho hicho hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi.

Ngeli ya kumi na nane ipo tu katika Kiswahili kati ya lugha mbili tunazozishughulikia. Haimo katika Kikikuyu.

Kiambisho cna jina katika ngeli hiyo ni {ma} ambayo haitokei katika kipande kingine chochote. Mofemu {mu} nuliwakilisha jina la ngeli hiyo kwenye sifa, vitenzi, vimiliki, na viashirio vya karibu na anayezungumza au mbali na anayezungumza pamoja na anayesikiliza. Mofemu {mo} huliwakilisha jina la ngeli hiyo kwenye ashirio la karibu na anayesikiliza na pia hutumiwa kama kijina kihusishi.

4.1.3 MISINGI YA KIMAANA

Kuna kufanana kwingi kati ya ngeli za Kiswahili sanifu na Kikikuyu kwa upande wa misingi ya kimaana.

Ngeli ya kwanza katika Kiswahili huyasheheni majina yote ya viumbe vyenye uhai. Lakini katika Kikikuyu, majina ya binadamu yanayoanza na {mu} ndiyo tu yaainishwayo katika ngeli ya kwanza. Majina ya binadamu na wanyama ambayo hayaanzi na {mu} yametawanyika katika ngeli kadhaa. Kwa mfano .

- a) Kuna baadhi ya majina ya wanyama ambayo yameainishwa katika ngeli ya tatu kama vile [morod̪i] "simba" [mori:o] "kinyonga mwenye pembe".
- b) Majina ya binadamu wenye ila za kimwili huainishwa katika ngeli ya saba. Kwa mfano [kjoɾɔɛ] "kiwete" [ɣetumumu] "kipofu" [kerimo] "juha". Baadhi ya majina ya wanyama pia huwa katika ngeli hiyo. Kwa mfano. [kjora] "chura", [kembu] "kinyonga", [kehruta] "kipepeo".
- c) Majina mengi ya wanyama huainishwa katika ngeli ya tisa. Kwa mfano;
[ɲɔndu] "kondoo", [ɲɔmbɛ] "ng'ombe", [mbori] "mbuzi"
[ɾɔɔɣu] "ndovu" na kadhalika.

Ngeli ya pili katika Kiswahili na Kikikuyu huwa na hali ya wingi wa majina yapatikanayo katika ngeli ya kwanza.

Majina ya miti inayonenepa yameainishwa kwenye ngeli ya tatu katika lugha zote mbili Kiswahili na Kikikuyu. Kwa mfano . [mnazi, msɔnɔbari, mɔɛra] na kadhalika, katika Kiswahili; na [motamaijo, moiri, mɔɔandoka] , na kadhalika, katika Kikikuyu. Aidha, majina ya vitu vya kimaumbili huainishwa kwenye ngeli hiyo katika lugha zote mbili. Kwa mfano. [msitu, mwɛzi, mɔtɔ] katika Kiswahili, au [motito, mwɛri, mwaki] katika Kikikuyu.

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya tano huwa na baadhi ya viungo vya mwili. Kwa mfano [iru] "goti" [iɣɛɣɔ] "jino" [injoro] "pua". Ngeli hiyo pia huyasheheni majina ya sehemu za miti katika lugha zote mbili, kwa mfano. [iɔango] "jani" [iɣoko] "ganda".

Tofauti ya kimaana iliyoko baina ya ngeli ya tano katika Kiswahili na ya Kikikuyu ni kwamba dhana ya ukubwa usio wa kawaida hutolewa kwenye ngeli ya tano katika Kiswahili. Jambo hilo halitokei kwenye ngeli hiyo katika Kikikuyu bali huwa katika ngeli ya saba.

Katika Kikikuyu, ngeli ya tano pia huwa na baadhi ya majina ya kidhahania. Kwa mfano [iɔero] "mzaha" [reɣiria] "fikira".

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya sita huusheheni wingi wa majina ya ngeli ya tano na pia huwa na baadhi ya majina ya vitu majimaji. Kwa mfano [ma:e] "maji" [maɣuta] "mafuta" [mata] "mate".

Katika Kikikuyu, ngeli ya sita ina sifa ya ziada kwa sababu huwa na majina yaliyo hali ya wingi wa majina ya ngeli ya kumi na nne na kumi na tano.

Kwa mfano:

- [maondo] "mambo" {mɔ:hɔrɔ} / na+ohɔrɔ / "habari" kutokana na [ondo] "jambo", [ohɔrɔ] "habari" (ngeli ya 14) - [maɣoro] "miguu" [mato] "masikio" [mɔ:kɔ] /ma+ɔkɔ / "mikono" kutokana na [koɣoro] "mguu" [ɣoto] "sikio" [ɣwɔkɔ] "mkono" (ngeli ya 15).

Ngeli ya saba katika lugha mbili tunazozishughulikia ina aina za majina yanayofanana sana kimaana. Kwa mfano. Ngeli hiyo ina majina ya vitu vinavyoundwa na kutumiwa na binadamu kama vile, [ɣete] , "kiti", [ɣetanda] "kitanda," [ɣeɣiko] "kijiko" [ɣeɣanori] "kitana" na kadhalika. Ngeli hiyo pia huwa na majina ya baadhi ya viungo vya mwili. Kwa mfano. [kɣara] "kidole" [keɣkɔ:ra] "kisugudi". Aina nyingine ya majina yanayoainishwa kwenye ngeli ya saba katika Kiswahili na Kikikuyu huwa yameundwa kutokana na vitenzi. Kwa mfano:

[kererɔ]	"kilio" kutokana na	[rera]	"lia"
[ɣekunekɔ]	"kifunik" kutokana na	[kuneka]	"funika"
[kehato]	"kifagio" kutokana na	[ha:ta]	"fagia"

Katika lugha zote mbili, ngeli ya saba pia huyasheheni majina yote ya lugha.

Ngeli ya saba katika Kiswahili, pia huonyesha dhana ya udogo usio wa kawaida. Kwa mfano:

[kijitu] ni udogo wa [mtu] (ngeli ya 1)

[kijiti] ni udogo wa [mti] (ngeli ya 3)

[tʃumba] / ki+umba / ni udogo wa [ɟumba] (ngeli ya 9)

Hali huwa kinyume katika Kikikuyu ambapo ngeli hiyo huonyesha dhana ya ukubwa usio wa kawaida.

Kwa mfano:

[kemonɔ] "jitu" ni ukumbwa wa [monɔ] "mtu" (ngeli ya 1)

[kemote] "jiti" ni ukumbwa wa [mote] "mti" (ngeli ya 3)

[keɟomba] "jumba" ni ukumbwa wa [ɟomba] "nyumba" (ngeli ya 9)

Ngeli ya nane katika Kiswahili na Kikikuyu huwa na majina yaliyo wingi wa yale yanayopatikana katika ngeli ya saba. Lakini majina ya lugha hayawekewi wingi.

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya tisa huwa na majina yaliyokopwa kutoka lugha nyingine. Kwa mfano:

[βaiθikiri] "baiskeli", [mbaθi] "basi"

[θu:ti] "suti" na kadhalika. Ngeli hiyo pia huyasheheni majina yote ya nchi katika lugha zote mbili. Baadhi ya majina ya vitu majimaji pia huainishwa kwenye ngeli ya tisa katika lugha hizo.

Kwa mfano:

[θiθino] "jasho" [θakame] "damu"

Ngeli ya tisa katika Kiswahili na Kikikuyu pia huwa na baadhi ya majina ya kidhahania. Kwa mfano

[ɲaraθu] "njaa", [ho:ni] "shibe", [ɲgaθo], "shukrani".

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya kumi huwa na wingi wa majina kutoka ngeli ya tisa. Lakini katika Kikikuyu, ngeli hiyo huwa na sifa ya ziada kwa vile huyasheheni baadhi ya majina ya kidhahania.

Kwa mfano:

[θoni] "aibu /fedheha", [ɲgarari] "mabishano"

[θa] "huruma", na kadhalika. Jina [θjana]

"watoto" liko katika ngeli ya kumi ingawa hali yake ya uchache [mwana] "mtoto" iko katika ngeli ya kwanza.

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya kumi na moja huyasheheni majina ya vitu virefu na vyebamba. Kwa mfano:

[roβaru] "ubavu" [roθwere] "unywele"

[robito] "ufito" [roreme] "ulimi"

Licha ya kuyasheheni majina ya vitu virefu na vyebamba, ngeli ya kumi na moja katika Kikikuyu huwa na baadhi ya majina ya kidhahania. Kwa mfano.

[romɛna] "uhasama / chuki" [rwembɔ] "wimbo"

Ngeli ya kumi na mbili hupatikana tu katika Kikikuyu kati ya lugha mbili tunazozishughulikia. Ngeli hiyo hutoa dhana ya udogo. Kama tulivyosema hapo awali, dhana ya udogo hutolewa kwenye ngeli ya saba katika Kiswahili sanifu.

Ngeli ya kumi na tatu huonyesha hali ya wingi wa majina ya ngeli ya kumi na mbili. Ngeli hiyo pia haimo katika Kiswahili.

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya kumi na nne huwa na baadhi ya majina yanayoundwa kutokana na vitenzi, sifa, au majina mengine. Kwa mfano;

[wɛndɔ] /o+ɛndɔ / "upendo" kutokana na kitenzi

[ɛnda] "penda"

[oʃaka] "urembo" kutokana na sifa [ʃaka] "rembo"

[okaβira] "ukabila" kutokana na jina [kaβira] "kabila"

Katika lugha zote mbili, ngeli ya kumi na nne pia huwa na majina ya vitu visivyohesabika lakini si majimaji. Kwa mfano;

[te:ri] "udongo" [motu] "unga"

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya kumi na tano huyasheheni majina yanayoundwa kutokana na vitenzi.

Kwa kuiambikisha mofemu {ku} katika Kiswahili au {ko} katika Kikikuyu, vitenzi hupewa sifa za majina.

Kwa mfano.

[koθa:ka] / ko+θa:ka / "kucheza" kutokana na [θa:ka] "cheza"
[komaka] "kushangaa" kutokana na [maka] "shangaa"
[korema] "kulima" kutokana na [rema] "lima" KOREMA
Korema

Licha ya kuwa na majina yanayoundwa kutokana na vitenzi, ngeli ya kumi na tano katika Kikikuyu pia huwa na majina ya baadhi ya viungo vya mwili. Kwa mfano;

[koθoro] "mguu" [θwoko] /ku+oko /
"mkono" [θoto] "sikio".

Katika Kiswahili na Kikikuyu, ngeli ya kumi na sita humaanisha sehemu au pahali halisi. Ka mfano;

[hando haha] "pahali hapa"

Katika lugha zote mbili, ngeli ya kumi na saba humaanisha mahali kwa jumla. Kwa mfano: [kondo θo:ko]
"mahali huku"

Ngeli ya kumi na nane hupatikana tu katika Kiswahili kati ya lugha mbili tunazozishughulikia. Ngeli hiyo huonyesha mahali ndani. Kwa hivyo hakuna ngeli ionyeshaya dhana ya undani katika Kikikuyu.

SURA YA TANO

5.1.0 HITIMISHO

Katika sura ya kwanza (sehemu 1.3) tulisema kwamba madhumuni ya tasnifu yetu ni kuzichunguza njia mbili zilizowahi kutumiwa katika uainishaji wa ngeli. Njia hizo mbili zikiwa ni uzingatifu wa viambisho vya majina, na pia uzingatifu wa misingi ya kimaana. Kisha tulisema kwamba tutazihakiki kauli zilizowahi kutolewa na baadhi ya wanasarufi waliowahi kuushughulikia mpangilio wa ngeli za Kiswahili na Kikikuyu au katika lugha za Kibantu kwa jumla.

Tumeichukua kila mojawapo ya ngeli za Kiswahili na Kikikuyu na kuitalii misingi yake ya kimaana. Kisha, tumejitahidi kujadili jinsi majina katika kila ngeli yanavyochukuana na vipande mbalimbali vya sarufi.

Vipande vya sarufi ambavyo tumevihusisha katika utafiti wetu ni viashiria, sifa, vitenzi, kijina kihusishi, idadi na vimiliki.

Kulingana na utafiti wetu, nyingi kati ya ngeli za Kiswahili na Kikikuyu zina sifa nyingi zinazofanana kwa upande wa maana ingawa zimetofautiana sana katika kiwango cha viambisho vya majina.

Tumeona kwamba ngeli ya kwanza katika lugha zote mbili ina majina ya binadamu. Kwa mfano

[mondo] "mtu" [moʃu:ri] "mzee", [motumia]
"mwanamke" na kadhalika.

Sifa za pamoja katika ngeli ya tatu ni kwamba
ina majina ya miti inayonenepa, vitu vya kimaumbile,
na mengine ya kidhahania.

Katika lugha zote mbili, Kiswahili na Kikikuyu,
ngeli ya tano ina baadhi ya viungo vya mwili kama
vile [ri:ʃo] "jicho" [iʃɛʃo] "jino", na kadhalika.
Ngeli hiyo pia ina majina ya sehemu za miti katika
lugha zote mbili. Kwa mfano [iʃango] "jani" [iʃo ko]
"ganda".

Katika lugha zote mbili, ngeli ya sita ina majina
ya baadhi ya vitu majimaji. Kwa mfano [ma:e] "maji",
[mata] "mate".

Ngeli ya saba katika lugha zote mbili ina vitu
vinavyoundwa na kutumiwa na binadamu, baadhi ya majina
ya viungo vya mwili, majina ya lugha, na pia majina
yanayoundwa kutokana na vitenzi.

Katika Kiswahili na Kikikuyu, tumeona kwamba ngeli
ya tisa ina majina yaliyokopwa kutoka lugha nyingine,
na pia majina ya nchi.

Ngeli ya kumi na moja katika lugha zote mbili
ina majina ya vitu vyebamba na virefu.

Katika lugha zote mbili, ngeli ya kumi na nne ina
vitu visivyoweza kuhesabika lakini si majimaji.

Ngeli hiyo pia ina majina yanayoundwa kutokana na vitenzi, sifa, au majina mengine.

Katika lugha zote mbili, tumeona kwamba ngeli ya kumi na tano ina majina yanayoundwa kutokana na vitenzi.

Katika lugha mbili tulizozishughulikia, ngeli ya kumi na sita yaonyesha pahali au sehemu halisi. Nayo ngeli ya kumi na saba yaonyesha mahali kwa jumla katika lugha zote mbili.

Kufanana kwingi kunakodhihirika kati ya ngeli za Kiswahili na Kikikuyu hakuwezekani kuwa ni jambo la sadifa. Kwa hivyo hatuna budi kuufikia uamuzi kwamba mpangilio wa ngeli katika lugha mbili tulizozishughulikia unatawaliwa sana na dhana ya maana.

Jambo lingine linaloambatana na mpangilio wa ngeli na ambalo lapasa kujadiliwa ni kuhusu uhusiano uliopo baina ya viambisho vya majina na mofemu zinazoyawakilisha majina kwenye vipande vingine vya sarufi.

Baadhi ya wanasarufi waliotutangulia, kama vile Barlow (1960:14) na Welmers (1973:171) wameichukua dhana ya takiriri kwa ujumla sana. Barlow anatoa jina [roɗapɗu] "mkongojo" (ngeli ya 11) kama mfano kuonyesha jinsi kiambisho {ro} kinavyokaririwa

kwenye vipande vingine vya sarufi ya Kikikuyu. Naye Welmers ametumia jina [kikapu] (ngeli ya 7) kama mfano ili kuonyesha takiriri katika Kiswahili.

Kauli za kina Barlow na Welmers zimewapotosha wanasarufi wa baadaye. Kwa mfano Mutisya (1986) amesema;

"Katika Kiswahili, viambisho vilivyoko kwenye majina hukaririwa kwenye vipande vingine vya sarufi isipokuwa katika ngeli ya tano"¹
(Tafsiri yetu)

Tumeonyesha katika tasnifu hii kwamba viambisho vya majina ya ngeli ya saba katika Kiswahili na kumi na moja katika Kikikuyu hukaririwa kwenye vipande vingine vyote vya sarufi katika sentensi. Hatubishani na wanasarufi tuliowataja hapo awali kuhusu jambo hilo. Lakini hatukubaliani nao kwamba takiriri ya aina hiyo hutokea katika kila ngeli.

Takiriri ya kiambisho cha jina kwenye vipande vingine vyote vya sarufi hutokea tu kwenye ngeli za saba na nane katika Kiswahili. Takiriri hutokea zaidi katika Kikikuyu, Katika lugha hiyo, ngeli zilizo na takiriri ni; 5,6, 7,11,12, 13, 15, 16, na 17. Kwa hivyo kauli za Barlow, Welmer, na Mutisya hazina mashiko.

Ukweli ni kwamba si lazima kiambisho kilichoko kwenye jina kikaririwe hivyo hivyo kwenye vipande vingine vya sarufi.

Kauli nyingine iliyowahi kutolewa kuhusu mpangilio wa ngeli ni kuweco kwa jozi za uchache na wingi.

Chambilecho Gromova (1983:30), hatuwezi kutoa kauli ya jumla kuhusu kuweco kwa jozi za uchache na wingi wa ngeli katika lugha mbili tulizozishughulikia. Hii ni kwa sababu kati ya ngeli za kila mojawapo ya lugha hizo, ni chache sana ambazo zaonyesha hali ya wingi. Kwa mfano; Kati ya ngeli kumi na sita za Kiswahili sanifu, ni ngeli tano pekee ambazo zaonyesha wingi. Ngeli hizo ni 2, 4, 6, 8, na 10.

Katika Kikikuyu, ngeli zinazoonyesha hali ya wingi ni sita pekee. Ngeli hizo ni 2,4,6,8, 10 na 13.

Tumeonyesha katika kazi yetu kwamba kuna uwezekano wa ngeli moja kuusheheni wingi wa ngeli kadhaa. Kwa mfano; katika Kiswahili, ngeli ya kumi inausheheni wingi wa majina ya ngeli ya tisa na ya kumi na moja.

Katika Kikikuyu, ngeli ya sita huwa na majina kutoka ngeli ya tano, kumi na nne, na pia kumi na tano. Nayo ngeli ya kumi katika lugha hiyo huwa na

wingi wa majina ya ngeli ya tisa na ya kumi na moja.

Jina [mwana] "mtoto" katika Kikikuyu huwa katika ngeli ya kwanza. Lakini ajabu ni kwamba wingi wake [Sjana], /Si+ana/ "watoto" huainishwa katika ngeli ya kumi.

Kulingana na maoni yetu na kama tulivyodhihirisha katika kazi hii, mpangilio wa ngeli za lugha mbili tulizozishughulikia watatanisha sana. Kwa hivyo yamfaa mtu anayeushughulikia ajihadhari dhidi ya kutoa kauli zozote za kijumla ambazo hazidhihiriki kisarufi.

5.1.1 MAPENDEKEZO

Tasnifu yetu imejikita katika sarufi linganishi ya Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu. Tulijishughulisha na ulinganishi wa ngeli katika lugha hizo mbili ambao ni kimoja tu baadhi ya vipengele vya sarufi linganishi.

Kuna mambo mengi ambayo yaweza kufanyiwa utafiti kuhusiana na lugha hizo mbili. Lakini hatungejishughulisha nayo kwa kuwa yako nje ya upeo wetu.

Ingefaa utafiti ufanywe kuhusu ulinganishi wa ngeli katika mojawapo ya lahaja nyingine za

Kiswahili kama vile Kiamu, na za Kikikuyu. Yumkini lahaja kama hiyo haijaathiriwa na lugha nyingine kama kilivyo Kiswahili sanifu. Kwa hivyo tungependa kujua kama lahaja hiyo inafanana au kutofautiana zaidi na Kikikuyu ikilinganishwa na Kiswahili sanifu.

Aidha utafiti ungefanywa ambapo lugha zinazohusika ni zaidi ya mbili. Matokeo ya data za lugha kutoka eneo mbalimbali yangetutolea mwanga zaidi na kutupa ujasiri tunapozitoa kauli za kijumla kuhusiana na uainishaji wa ngeli za Kibantu.

TANBIHI

1. Mutisya, J. (1986) Concordial Agreement in
Kiswahili and Kikamba:
A Comparative Analysis.
Tasnifu ya B.A.
Chuo Kikuu cha Nairobi
(Bado haijachapishwa) uk. 46

MAREJELEO

- Ashton, E.O. (1944) Swahili Grammar: London,
Longman.
- Bakari, M. (1982) The Morphophonology of the
Kenyan Swahili Dialects:
Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu cha
Nairobi. (Bado haijchapishwa)
- Barlow, A.R. (1960) Studies in Kikuyu Grammar and
Idiom; Edinburg; William
Blackwood and sons Ltd.
- Bennet, P.R. (1970) "The Problem of Class in Kikuyu"
Makala katika African Language
Studies. Juzuu La x, kurasa 48-59
- (1986) "Grammar in the Lexicon"
Makala katika Journal of African
Languages and Linguistics.
Juzuu la 8/1; Dordrecht; Foris
Publications. kurasa 1-30.
- Bleek, W.H.I (1869) Comparative Grammar of South
African Languages; London;
Tübingen and Company.
- Brain, J.L. (1966) Basic Structure of Swahili.)
Syracuse; Syracuse University
Press.

- Broomfield, G.W. (1931) Sarufi ya Kiswahili;
London, The Sheldon Press.
- Burt, F. (1917) Swahili Grammar and
Vocabulary (Toleo la 2),
London; Society for
Promoting Christian Knowledge
- Denny, J.P. na C.A. Greider, (1976 a) "The Semantics
of Noun Classes in Proto
Bantu" makala katika African
Linguistics. Juzuu la 7/1
----- (1976b) "What are noun classes Good
for?" Research Bulletin
No. 365, may 1976,
Department of Psychology;
University of Chicago.
- Der-Houssikian, H. (1979) Noun Class and Concord in
Kimombasa. Tasnifu ya Ph.D
Chuo Kikuu cha Texas, Austin.
- Driever, D. (1973) "Some Notes for Discussion
on Problems of a Case Grammar
in Swahili" Institute of
African Studies, University
of Nairobi, Discussion Paper
No. 49.

- Ford, K.G. (1974) Tone and Intonation in Kikuyu; Nairobi, University of Nairobi.
- Gathenji, W.H. (1981) The Morphology of the Verbal Extensions in Gikuyu - A Functional Approach, Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Gecaga, B.M. na W.H. Kirkaldy (1953) A short Kikuyu Grammar; London Macmillan and Company Ltd.
- Gibbe, A.G. (1983) "Uchambuzi wa Nomino za ngeli ya kwanza" makala katika Lugha ya Kiswahili; Dar-es-Salaam; Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. kurasa 244-256
- Givon, T. (1971) "Some Historical changes in the Noun Class System of Bantu, Their possible causes and wider Implications" makala katika Kim Chin-Wu na Stahlke, H (Wahariri) Papers in African Linguistics; Edmonton; Linguistics Research Inc. kurasa 33-54.

- Gromova, N. (1983) "On Correlation of the Categories of class and Number in some Bantu Languages" makala katika Kiswahili Toleo la 50/1, Dar-es-Salaam; Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili; kurasa 29-32.
- Hassan, M.M. (1973) Fuseme Kiswahili. Berkley; Simba Publishers.
- Henrici, A. (1973) "Numerical Classification of Bantu Languages" makala katika African Language Studies. Juzuu la xiv, London; School of Oriental and African Studies; kurasa 83-104
- ↳ Hinnebusch, T.J. (1975) "A Reconstructed Chronology of Loss: Swahili Class 9/10" makala katika Herbert, R. K (Mhariri) Proceedings of the Sixth Conference on African Linguistics; Columbus; Chuo Kikuu cha Ohio; kurasa 32-41
- International Phonetic Association (1949) The Principles of International Association; London, University College.

- Johnson, H.W. (1919) A Comparative Study of the Bantu and Semi Bantu Languages. London; Oxford University Press.
- Kapinga, M.C. (1983) Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Dar-es-Salaam; Printpak (Tanzania) Ltd.
- Kenya Government (1979) Kenya Population Census, Juzuu la kwanza; Nairobi; Government Printers.
- Krapf, J.L. (1882) A Dictionary of Swahili Language. London; Tübingen and Company.
- Leakey, L.S.B. (1959) First Lessons in Kikuyu. Nairobi East African Literature Bureau.
- Loogman, A. (1965) Swahili Grammar and Syntax, Pittsburgh; Duquesne University Press.
- Masoko, M. (1983) "Maana na mpangilio wa Umbo "ki" katika Kiswahili" makala katika Kiswahili. Toleo 50/1 Dar-es-Salaam, TUKI.
- Matthews, P.H. (1974) Morphology: An Introduction to the Theory of Word Structure London, Cambridge University Press.

- Mbaabu, I (1978) Kiswahili: Lugha ya Taifa
Nairobi, Kenya Literature
Bureau.
- (1985) Sarufi ya Kiswahili. Nairobi,
Kenya Publishing and Book
Marketing Company.
- Mdee, J.S. (1986) Kiswahili: Muundo na Matumizi
yake. Nairobi Intercontinental
Publishers Ltd.
- Mfaume, G.E. (1984) Misingi ya Isimu ya Lugha ya
Kiswahili. Dar-es-Salaam;
Printpak (Tanzania) Ltd.
- Mutahi, E.K. (1977) Sound Change and the Classification
of the Dialects of Southern
Mt. Kenya; Tasnifu ya Ph.D,
Chuo Kikuu cha Nairobi.
(Ilichapishwa 1983)
- Mutisya, J. (1986) Concordial Agreement in Kiswahili
and Kikamba. A Comparative
Analysis. Tasnifu ya B.A. Chuo
Kikuu cha Nairobi. (Bado
haijachapishwa)
- Myachina, E.N. (1981) The Swahili Language. London,
Routledge and Kegan Paul Ltd.

- Myer, A. (1972) "The making of an Exception: A curious Non-application of Dahl's Law in Kikuyu" makala katika Voeltz, E. (Mhariri) Third Annual Conference on African Linguistics, 7th-8th April 1972, Bloomington, Indiana University, kurasa 135-138
- Njoroge, D.N. (1978) Kikuyu Deverbatives and other Nominalizations; Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi; (Haijachapishwa) ✕
- Polome, E.C. (1967) Swahili Language Handbook. Washington D.C., Center for Applied Linguistics.
- Salin, A.I. (1973) The Swahili - Speaking Peoples of Kenya's Coast 1895-1965. Nairobi; East African Publishing House.
- (1974) "Native or non-native? The Problem of Identity and the Social Stratification of the Arab-Swahili of Kenya's Coast" Makala katika Ogot, B.A. (mhariri) History and Social Change in East Africa. Nairobi, East African Literature Bureau

- Slavicka, M. na M.A. Bryan (1973) "Comparative Bantu: The case of two Swahili Dialects" makala katika African Language Studies, Juzuu la xiv kurasa 53-81
- Stigand, C.H. (1915) A Grammar of Dialect Changes in Swahili. London, Cambridge University Press.
- Tucker, A.K. na M.A. Bryan (1957) Linguistic Survey of the Bantu Borderland. Juzuu la nne, London: Oxford University Press.
- Wa Mberia, K. (1979) The Morphology of Kitharaka Nominal Word. Tasnifu ya B.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Bado haijachapishwa). ×
- Welmers, W.E. (1973) African Language Structures Los Angeles, University of California Press.
- Wilson, P.M. (1970) Simplified Swahili. Nairobi, East African Literature Bureau.
- Zawawi, S.M. (1979) Loan Words and Their Effect on the Classification of Swahili Nominals. Leiden, E.J. Brill.